**5 JUNI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### Kikao cha Arobaini – Tarehe 5 Juni, 2025

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025)*.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025)*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu kwa heshima na taadhima. *(Makofi)*

Tutaanza na Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kazi njema ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo inafanywa kwenye Kitengo chako cha Maafa. Tumeona kwa namna ambavyo aliwasaidia wenzetu kule Hanang, Rufiji, Mbeya na maeneo mengine yaliyopo hapa Tanzania, kazi yake ni njema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kadhia hii imekuwa ikiendelea kuwakumba Watanzania wengi kupata maafa kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini kwetu na hivyo kupoteza makazi, kupoteza maisha na wakati mwingine mashamba yao kuharibiwa na kupoteza vyakula. Pia Kamati zetu za Maafa zilizopo kule za Wilaya na Mikoa, wakati mwingine hazina uwezo wa kuyamudu maafa haya na kuwahudumia Watanzania hawa kwa kadri ambavyo inatakikana ikiwemo kuwarejeshea mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ipi kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu maafa haya yanapokuwa yanatokea aidha kuziwezesha Kamati za Wilaya na Mikoa ziweze kutatua changamoto hii au yeye kuona namna ya kuwasaidia kwa haraka maafa haya yanapotokea, kupata makazi na kurejeshewa vyakula kwa haraka kama ambavyo wanaona maeneo mengine

yanahudumiwa ili kuweka matumaini kwa Watanzania ambao wanakuwa wamekosa misaada kwa haraka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya njema leo tunakutana tena kwenye Bunge tukiendelea na majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Sichalwe, Mbunge wa Momba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru kwa kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla kwa jitihada mbalimbali zinazochukuliwa kukabiliana na maafa yanayoendelea hapa nchini kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu kama mratibu wa maafa nchini imeweka utaratibu unaoweza kupata taarifa za maafa yoyote yale mpaka ngazi za vijiji. Tumeunda Kamati za Maafa kuanzia ngazi ya kijiji, kata, halmashauri (wilaya), mkoa na ile ya kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya kamati hizi ni kwanza kubaini tatizo linapojitokeza na kuharakisha kutoa taarifa kwenye ngazi yake ya juu. Unajua maafa haya yanatokea kwanza kwenye ngazi ya vijiji, unakuta kuna maporomoko kwenye eneo la vijiji kwa hiyo Kamati zile zinatoa taarifa. Tunajua hazina uwezo mkubwa wa kushughulikia baadhi ya maafa, lakini kuweka itifaki zile inasaidia utoaji wa taarifa na uelezaji wa ukubwa wa tatizo na ukubwa wa tatizo unasaidia pia ngazi husika kuweza kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kazi kubwa ambayo sasa tunaifanya ni kuziimarisha kamati hizi kwa kuzipa elimu na kuzipa mifumo ambayo unaweza kutoa taarifa kwa haraka kwenda kwenye kamati za juu. Pia zinapotokea kwenye ngazi ya kijiji na wilaya unajua Mkuu wa Wilaya ndiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Maafa ngazi ya Wilaya anachukua hatua na anapoona aina hiyo

ya maafa imemzidi nguvu anatoa taarifa mkoani na baadae Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uimarishaji wa kamati hizi ni pale ambapo tunawapa elimu juu ya kukabiliana na maafa. Tunajua yanatofautiana, lakini angalau wanakuwa na elimu ya kukabiliana na maafa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kuwa ngazi ya mkoa na Taifa inachukua muda kupeana taarifa na kuwahi, tumeamua kuanzisha maeneo ya kimkakati kwenye ngazi za kanda ambazo leo hii tumeamua pia kupeleka vifaa mbalimbali kwenye maeneo haya ya kanda iwe rahisi kuwasiliana na mkoa na kufika kwenye maeneo kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama vile ilivyotokea Hanang, kanda yetu ipo Arusha, walipopata tatizo lile na ngazi ya mkoa wakaona tatizo hili ni kubwa zaidi walitoa taarifa Arusha, Arusha wakawajulisha Makao Makuu. Kwa hiyo, sisi tulipokuwa Rufiji tunapata taarifa kwamba huku kuna tatizo kubwa, tayari Arusha walishafika *site* na kuanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo huo ndiyo mfumo ambao tunautumia wa hatua hizi na uimarishaji wake kwa kuweka maghala ya kuweka vifaa vya maafa kwenye maeneo ya kanda ili iwe rahisi kuzifikia mikoa na wilaya huku tukiwa tumeimarisha kamati zile kuwa na uelewa wa namna ya kutoa taarifa na kukabiliana na matatizo ambayo yanajitokeza kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niwahakikishie Watanzania, Serikali imejipanga kwenye eneo hili baada ya kuwa tumepata matukio mengi ya maafa. Tumenunua vifaa vingi ambavyo vinaweza kusaidia kwa awali kulingana na tukio linavyojitokeza na kamati zetu tayari zina uelewa na tunaendelea kuelimisha kamati hizi ili ziwe na uwezo wa kukabili matukio haya kwa haraka sana na hatimaye tuweze kuokoa maisha ya watu wetu, mali zao na mashamba kama alivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo hatua tuliyoichukua sasa hivi Serikali kuimarisha na kukabiliana na maafa, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante. Ninamwita Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii adhimu na muhimu kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali nikitegemea kwamba haitokuwa ya mwisho, *In Shaa Allah! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imewekeza kwa gharama kubwa sana katika mradi mmoja muhimu sana wa treni ya *SGR* ambao umeenda kuwa mkombozi kwa wananchi wote ambao wanategemea usafiri na kwa kweli ni nafuu sana kulinganisha na gharama zake ukilinganisha na ndege. Hata hivyo, kumekuwa na safari chache za kutoka *station* za Magufuli, Dar es Salaam hadi Dodoma, *Samia Suluhu Station* na kutoka *Samia Suluhu Station* hadi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi sana wanategemea fursa hii ambayo ni mkombozi mkubwa hasa kwa unafuu wake, lakini safari zenyewe zimekuwa chache.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuziongeza ratiba za safari hizi ili wananchi wanapohitaji waweze kupata usafiri kwa urahisi na hasa wakitegemea kama huu ndiyo ufumbuzi wa tatizo lao sugu la usafiri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi unaweza kulala Dodoma ukaenda kunywa chai Zanzibar saa nne ya usiku. Unafika saa tatu unapanda boti ya saa 3.30 unafika Zanzibar saa 4.00 au 5.00, kuna kubwa zaidi ya hilo? Nani kama Mheshimiwa Mama Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninataka Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake na hasa kwa vile watendaji wote na Waziri wanaoshughulikia masuala haya ya *SGR* wamefanya vizuri sana,

waziongeze hizi safari kwani tunazihitaji na kesho kutwa tunataka kwenda kwenye Eid. ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Asha almaarufu kama Mheshimiwa Mshua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwamba ameipongeza Serikali na amempongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hatua hii iliyofikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu tulianza awamu ya tano chini ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli na baada ya Mheshimiwa Dkt. Samia kuingia madarakani mmeona hatua hizi ambazo tumezipitia na leo hii Mheshimiwa Rais ameshazindua safari na safari zimeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatua hizi zote zinazoendelea tunakwenda kuimarisha usafirishaji kwa njia ya treni kutoka Dar es Salaam na lengo ni kufika Mwanza, Kigoma, Mpanda mpaka Kalemie. Kwa hiyo, hatua ambayo tumeianza sasa Dar es Salaam, Morogoro, na Dodoma ya kusafirisha abiria tayari safari zimeshaanza na tulianza na safari mbili kwa siku, kutoka Dar es Salaam safari mbili, kuja Dodoma na Dodoma kwenda Dar es Salaam safari mbili huku kukiwa na safari za Dar es Salaam Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ambazo zipo mezani kwangu, Wizara iliahidi kuongeza safari mpaka nne. Sijafuatilia, kama ningepata muda wa kufuatilia ningeweza kukuambia leo tuna safari ngapi lakini tayari walishatuandikia kwamba wanatarajia kuongeza safari kufikia nne ili kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma kuwe na treni nne. Malengo walisema asubuhi mapema, saa nne, saa nane na saa 12 kutoka pande zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya ni maboresho na ni hatua nzuri hivyo tuendelee kuwa na matumaini kwamba Serikali

inatambua hili na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge mmeshatoa mapendekezo; ninachukua kama mapendekezo kwamba tuongeze safari kwa sababu ya uhitaji mkubwa.

Niwahakikishie, tunapokwenda ni kuzuri zaidi, kutakuwa na safari nyingi zaidi na hasa wakati huu ambapo tumeanza safari za mwendokasi kupitia ile *tube*, (ule mchongoko), tunataka tuongeze na safari za mchongoko vilevile ambazo zinatoka Dar es Salaam mpaka Dodoma moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwahakikishie Watanzania uimarishaji wa treni unaendelea na uongezaji wa safari utaimarika. Tunaangalia sasa uhitaji huu na idadi ya abiria wanaokwenda huko ili tuweze kuanza safari hizo na kuimarisha safari hizo, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu sahihi. Sasa ninamwita Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu limebahatika kuwa na mito mingi, maziwa pamoja na bahari jambo ambalo limepelekea wananchi wengi kuona fursa kupitia maeneo haya. Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hii ya uvuvi katika kukuza uchumi wa bluu; je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inaweka mazingira ya upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wavuvi wetu wa wajasiriamali kwa mazao ya baharini ili kukuza na kuendeleza uzalishaji wa mazao ya baharini kupelekea kuwa na thamani ya mazao hayo pamoja na ajira kwa watu wetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Simai, Mbunge kutoka Zanzibar kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia sekta ya uvuvi na namna ambavyo wajasiriamali wetu wakiwemo wavuvi wenyewe wanavyoshiriki kikamilifu katika kujipatia kipato, lakini Mheshimiwa Mbunge ameonesha kuwa yapo mapungufu kidogo ya wanaotamani kwenda kuingia kwenye sekta ya uvuvi kukosa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni kwamba sekta hii Serikali zetu zote mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tumeweka kwenye sera kabisa ya uchumi wa bluu na kuendesha hamasa ya Watanzania wanaotaka ambao pia tayari walishaanza shughuli za uvuvi kuendelea na kuwatia imani kwamba Serikali inaweka mpango endelevu wa kuwafanya wao washiriki kikamilifu kwenye shughuli ya uvuvi ili waweze kujipatia kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua, tuna wavuvi wenyewe na uhitaji wao, tuna wajasiriamali ambao wanashughulika na uchakataji wa mazao ya baharini, kwenye mito na maziwa yetu; hao wote tumewaratibu vizuri. Suala la mikopo, ninataka niwape faraja wale wote walioanza na wanaotaka kuanza kuingia kwenye sekta ya uvuvi, Serikali imezungumza na taasisi za fedha (benki) ikiwemo Benki ya Kilimo *(TADB)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa karibuni tumezindua Benki ya Ushirika (wavuvi wana ushirika wao na wana benki sasa) na Benki ya Biashara *(TCB)* iliyopo chini ya Serikali kwa asilimia zote. Pia tuna hizi benki kama *NMB, CRDB, NBC,* Azania na *Mkombozi Bank* hizi nazo ni benki ambazo tayari tumezungumza nazo na wameshatekeleza maelekezo ya Serikali ya kufungua dirisha kwa ajili ya kutoa fursa za wajasiriamali, sio wavuvi tu, hata wafugaji kwenye sekta ya kilimo, na wafanyabiashara wadogo wadogo, hawa wote wana nafasi ya kwenda kukopa pamoja na wakina mama lishe na baba lishe. Wote hawa wanapata mikopo kutoka ile midogo, ya kati mpaka mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu nenda kaeleze mpango wako wa biashara, unataka kufanya nini? Utekelezaji wake upoje? Pato lako litakuwaje? Je, una uwezo wa kurejesha mkopo? Ukishakamilisha haya unapata mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilitaka niwahakikishie Watanzania ambao wanapanga mpango wa kwenda kuingia kwenye ujasiriamali wowote ule ikiwemo na uvuvi kwamba fursa ya kupata mikopo ipo, si tu taasisi za kifedha, lakini tuna mifuko hii ambayo tunayo Serikalini ikiwemo na ule wa halmashauri wa 10% wa wanawake, vijana na walemavu. Pia tuna mifuko mingine inayolenga kada tofauti kupitia Idara ya Uwezeshaji iliyopo Ofisi ya Waziri Mkuu, ni maeneo ambayo Mtanzania yeyote anayetaka kuanza biashara anaweza kupata mkopo na akaamua kwenda kuanza biashara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu, ukikopa lipa mkopo ili umwezeshe na mwingine kuweza kukopa mkopo huo. Kwa hiyo, huu ndiyo mpango wa Serikali ambao tunao wa kuwezesha wajasiriamali kufanya kazi zao, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Jacqueline Andrea.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niweze kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya kazi kubwa ya kuimarisha huduma za afya nchini hadi ngazi za vijiji. Sambamba na huduma hizo, kumekuwa na uhitaji mkubwa wa madaktari bingwa wa magonjwa ya akina mama pamoja na watoto kwa ngazi za wilaya pamoja na vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limeathiri upatikanaji wa huduma bora za akina mama wajawazito pamoja na watoto wachanga. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha wilaya zote zinapata madaktari bingwa mpaka ngazi za vituo vya afya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline, Mbunge wa Tabora, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali wa kuhakikisha kuwa huduma za afya zinatolewa kwa uhakika na usahihi ni; moja, tunaendelea kuwasomesha Watanzania kwenye vyuo mbalimbali katika kada mbalimbali kwa sababu, huduma za afya ziko kada mbalimbali. Vilevile wako madaktari kwenye kada mbalimbali, lakini kuna wauguzi na wale watoa huduma za afya ambao tunawapeleka vijijini kushirikiana na kamati za afya za vijiji ili kutambua na kubaini magonjwa ya mlipuko na magonjwa mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo tunaliimarisha ni baada ya kuwa tumewasomesha hawa, tunawaajiri na nataka nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutoa vibali vya ajira vya kada ya sekta ya afya huku tukienda sambamba na uwezeshaji wa ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika zahanati, vituo vya afya, hospitali za halmashauri za wilaya, mikoa na huku juu kwenye hospitali za rufaa, ikiwemo Benjamini William Mkapa. Ni uwezeshaji ambao umefanywa vizuri na ni uwekezaji mkubwa sana kwenye miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira hizi ambazo Mheshimiwa Rais anaruhusu kutoa vibali ili kuwaajiri madaktari wakiwemo na hao madaktari bingwa wa magonjwa ya mama na mtoto na pia wa upasuaji, sasa hivi tunawapeleka mpaka vituo vya afya. Vilevile tuna madaktari bingwa wa mambo ya mdomo, masikio na macho; wote hawa sasa tunawapeleka mpaka ngazi ya Wilaya, ili huduma hizi zitolewe kwenye eneo hilo. Kwa, hiyo, mkakati wa Serikali wa kupeleka madaktari bingwa upo na ajira zinaendelea kutolewa ingawa siyo nyingi, ni kulingana na uhitaji na uwezo wa fedha wa Serikali, lakini vibali vinatolewa na vinaajiri. Sasa agizo ambalo tumelitoa kwa Waganga Wakuu wa Mikoa ni kuhakikisha ikama ya madaktari inapitiwa wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni, kuondoa mlundikano wa madaktari hao bingwa kuwa sehemu moja na kukosekana katika maeneo, kama vituo vya afya, ili waweze kusambazwa maeneo yote na huduma ziendelee kama kawaida.

Kwa hiyo, mkakati huu tunaendeleanao, wa kuimarisha ajira na kuwasomesha zaidi na wale waliopo kuwapa elimu ya mara kwa mara, ili waweze kutoa huduma stahiki kwenye maeneo yote, yakiwemo maeneo ambayo umeyaeleza Mheshimiwa Mbunge ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaendelea kuimarisha sekta ya afya. Leo hii huduma ambayo inatolewa ni ya kupunguza gharama za wananchi, ili huduma wazipatie hukohuko waliko. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Emmanuel Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, mimi natoa shukurani kubwa. Naipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Sita kwa kusimamia vizuri viwanda na ushirika hapa nchini, lakini pia nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, umekuwa kinara mkubwa wa kurejesha viwanda vya wanaushirika hapa nchini, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, hayo makofi, Mheshimiwa Waziri Mkuu hasikii na mimi sisikii huku. Muacheni aseme. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni nini sasa mkakati mahsusi wa Serikali kuwezesha ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani hapa nchini, hasa katika mazao ya kibishara mfano pamba, tumbaku, kahawa, korosho na mazao mengine muhimu, ili kuweza kuwanufaisha zaidi wakulima wetu? Ikiwezekana wakulima hawa waweze kulipwa malipo ya ziada, malipo ya pili, ili waone thamani ya mazao yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cherehani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa kuongeza viwanda nchini; moja, unatokana na sera tuliyonayo ya ujenzi wa viwanda kwa kuwakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuja kuwekeza hapa nchini. Wito huu unatokana pia na maboresho makubwa tuliyoyafanya ya kuweka mazingira wezeshi ya wawekezaji kufurahi kuamua kuja kuwekeza nchini wakiamini kwamba watapata faida, lakini pia na sisi Serikali tutanufaika na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza kurekebisha changamoto ambazo wawekezaji wengi wamekuwa wakizilalamikia ili kufungua milango ya wawekezaji wengi kuja na kuondokana na changamoto hizo kwa hiyo, mkakati huu tunaendeleanao. Pia hata Mheshimiwa Rais aliamua kuunda Wizara maalum, Wizara ya Mipango na Uwekezaji, iliyoko chini ya ofisi yake na tuna taasisi yetu ya *TAC;* Taasisi ya Uwekezaji nchini, ambayo yenyewe kazi yake ni kutangaza fursa mbalimbali zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, msisitizo tunaouweka hapa ni viwanda vinavyoweza kuchakata mazao ambayo tunayazalisha katika kilimo, likiwemo zao la pamba, korosho, chai, kahawa na mengine yaweze kuongezewa thamani, ili wakulima wetu waweze kupata faida. Mkakati huu umewezesha mambo mengi sana na tumepata unafuu pia, hata wa kilio cha ajira ambacho tunacho nchini. Tuna Watanzania wengi wanapata nafasi ya kuajiriwa kwenye viwanda hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna hamasisha sana uwekezaji wa ndani ambapo tumeweza kutoa fursa za kwa kuwapunguzia gharama ya mtaji wa kuwekeza kwenye viwanda. Mwanzo tulikuwa na uwekezaji wa ndani, mtu anayetaka kujenga kiwanda mtaji ulikuwa ni dola 100,000, sasa hivi ni dola 50,000 kwa Watanzania. Tunataka tujenge uwezo wa Watanzania wenyewe kuweza kuwekeza katika kujenga viwanda vinavyochakata mazao ambayo tunayao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeweza kupeleka umeme kama nishati ya kuwezesha kuendesha viwanda na maji. Mmeona miradi mingi ya umeme mpaka vijijini na miradi mingi

mikubwa ya maji tunaendelea kuijenga. Malengo ni yeyote anayeamua kujenga kiwanda asipate shida kwenye eneo la upatikanaji wa umeme na hata maji pia ili kuendesha viwanda vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira haya tunaendelea kuyaeleza kwenye maeneo mbalimbali. Hivi karibuni tumetoka Japan ambapo tulikuwa tunahamasisha wawekezaji kutoka nchi hiyo kuja Tanzania kuwekeza. Tunafanya hivyo kupitia Balozi zetu, kuwa na makongamano na mijadala ya viwanda na uwekezaji kwa Watanzania na wafanyabishara wa Tanzania na wa nchi mbalimbali ili kuja Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama mpango, upo na tunaendeleanao na tutahakikisha tunasambaza viwanda hivi kulingana na upatikanaji wa mazao, ili uchakataji ufanywe hukohuko uzalishaji ulipo, ili kuweza kuwarahisishia wakulima wetu na wale waendeshaji wa viwanda kupata malighafi kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie wawekezaji wote kuja Tanzania kuwekeza kwa sababu Tanzania ni nchi ambayo imebahatika na imekaa kimkakati zaidi. Ina nchi nane jirani zinategemea soko za Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania iko kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na ina idadi kubwa ya wateja. Tanzania iko kwenye nchi za *SADC*, kuna idadi kubwa ya wananchi wanaotegemea soko la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa Bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pia unawapa nafasi ya kuweza kupeleka bidhaa kwa ukaribu kwenye nchi zao. Kwa hiyo, Tanzania ni mahali sahihi pa uwekezaji. Mazingira haya tunaendelea kuyatamka wakati wote na kuwahakikishia kwamba, akiwekeza Tanzania hatajuta. Watanzania mnajua hii ndiyo njia tunayopata mapato, tunaongeza ajira na mambo mengine ambayo yananufaika kupitia uwekezaji huo, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na huyo ndiyo Mheshimiwa Mbunge wa mwisho aliyepangwa kwenye maswali yako.

Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uwezo, umahiri na utayari wako kutumikia Taifa lako, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, juzi nilikuwa nazungumza na kiongozi mmoja wa *TRC*, wana mpango sasa wa kuleta treni Dodoma itakayotumia saa mbili na dakika 45 tu, hili ni jambo la kupongezwa sana kwa Serikali ya Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikuombe vilevile kama wataweza kubadilisha ratiba, treni zao ziingie Dodoma saa 1.30 asubuhi na ikitoka hapa iingie Dar es Salaam saa 1.30 asubuhi, itasaidia sana kukuza uchumi na kuhakikisha viongozi wa Kiserikali, Wabunge na watumishi wanawahi shughuli za Kiserikali kwa muda unaotakiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 512

### Kituo cha Afya Buzuruga Kuwa Hospitali

**MHE. MARY F. MASANJA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakipandisha hadhi Kituo cha Afya Buzuruga kuwa hospitali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Buzuruga hakina miundombinu ya kutosha kuwa hospitali. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2025 Serikali imeshatoa shilingi bilioni 3.1 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Ilemela ambapo jumla ya majengo 14 yamekamilika na hospitali imesajiliwa na inatoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kuendelea kuboresha miundombinu ya Kituo cha Afya Buzuruga, ili kuendelea kutoa huduma katika ngazi ya kituo cha afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masanja.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo imeendelea kuboresha miundombinu ya afya na hivi sasa wananchi wengi wanapata huduma bora katika vituo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza ni lini sasa Serikali itaongeza majengo ya ghorofa kwa sababu Kituo cha Afya cha Buzuruga kinahudumia watu zaidi ya *capacity* iliyopo, kwa mfano, vitanda viko 74, lakini wananchi wanaohudumiwa *OPD* ni wananchi 150, lakini pia akinamama wanaokwenda kujifungua katika Kituo hicho cha Afya Buzuruga ni takribani 550 mpaka 600 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo hiki ni lango la wilaya karibu tatu zinazopata huduma katika kituo hicho, ambazo ni Wilaya ya Ilemela, Magu na Nyamagana.

Ni lini sasa Serikali itaongeza majengo kwa kiwango cha ghorofa ili huduma za mama na mtoto pamoja na wodi za wazazi ziweze kuongezwa ili wananchi waendelee kupokea huduma bora ya afya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni lini Serikali itaongeza watumishi katika kituo hicho, ili wananchi waendelee kupokea huduma bora ya afya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Serikali iliandaa mwongozo na michoro ya ujenzi kulingana na maeneo husika vilipo vituo vya afya vya miji na majiji. Maeneo haya mara nyingi yana maeneo madogo, kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya chini. Kwa hiyo, mwongozo ambao umetolewa una ramani za maghorofa na majengo ya chini, lakini pia, tunatoa nafasi kwa halmashauri husika ku-*design* michoro ambayo itakuja kuthibitishwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kulingana na eneo walilonalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii nimuelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kumtuma Mganga Mkuu wa Halmashauri na *Engineer* wa Halmashauri, lakini pia Mganga Mkuu wa Mkoa, waende wakaone Eneo la Kituo cha Afya cha Buzuruga. Waone uwezekano wa kuchora michoro ambayo itakubaliana na eneo lililopo, kwa sababu eneo ni dogo, na kuwasilisha Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ajili ya kuona uwezekano wa kuanza kujenga majengo ya kwenda juu ili kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali imeendelea kuajiri watumishi wa sekta ya afya na katika kipindi cha miaka hii minne, 2021 mpaka sasa 2025, Serikali imeshaajiri wataalam wa sekta ya afya 34,720 ambao wamepelekwa kwenye halmashauri zote, kote nchini ikiwemo Halmashauri ya Ilemela. Nakuhakikishia Mheshimiwa Mary Masanja, Serikali itaendelea kutoa kibali na kipaumbele kwa Manispaa ya Ilemela na halmashauri zote ili kuhakikisha watumishi wanaendelea kuajiriwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda, ajiandae Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, mimi nauliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Kitunda kimezidiwa kabisa na idadi ya wagonjwa wanaokwenda pale, maana wanatoka mikoa mitatu, Tabora, Katavi na Mbeya. Inafikia hatua kitanda kimoja kinakuwa na wagonjwa wanne; je, lini mtapanua huduma kwenye Kituo cha Afya cha Kitunda? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, moja ya utaratibu wa Serikali na katika miongozo tinafanya utaratibu wa kupanua majengo ya vituo vya afya kulingana na mahitaji. Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Kakunda tutakwenda kufanya tathimini ya idadi ya wagonjwa wanaotibiwa katika kituo hicho cha afya kwa siku na kwa mwezi na kuona *gap* ya miundombinu ya wodi na majengo mengine, ili Serikali iweze kuingiza kwenye mpango wa kuongeza majengo na kuboresha huduma za afya katika eneo hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga, ajiandae Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, naishukuru Serikali kwa kutujengea hospitali ya wilaya, ambayo iko upande wa Jimbo la Ismani, lakini bahati mbaya wananchi wa Jimbo la Kalenga ambao mimi ni mtumishi wao wa sasa na wa baadaye, hawafiki kule.

Je, ni lini sasa Serikali itafikiria kutujengea hospitali ndogo katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Vijijini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ina hospitali ya halmashauri ambayo Serikali ilipeleka zaidi ya shilingi

3,800,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo na imekamilika na imeanza kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa mujibu wa Sera na Mwongozo wa Wizara ya Afya, kila halmashauri ina hospitali moja ya halmashauri, lakini pamoja na hospitali za halmashauri kuna fursa ya kujenga vituo vya afya vya kimkakati katika kata za kimkakati ili kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kiswaga, tutaendelea kuona namna ya kuboresha zaidi vituo vya afya vilivyopo katika Jimbo la Kalenga, lakini pia kujenga maeneo mengine ya kata za kimkakati, ili kusogeza huduma za afya karibu zaidi katika vituo hivyo vya afya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza, naishukuru Serikali kwa kutujengea zahanati kwenye Kata ya Bondeni na leo tunaenda kuweka jiwe la msingi, lakini kata hii haina kituo cha afya. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo cha afya kwenye Kata ya Bondeni, Jimbo la Hai? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujenga vituo vya afya kwenye kata kuna vigezo ambavyo vimeainishwa; moja, ni idadi ya wananchi katika kata husika, lakini pili ni umbali kutoka kituo cha jirani zaidi cha afya.

Kwa hivyo, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kupata fedha, kwa ajili ya kujenga zahanati katika Kata ya Bondeni, lakini nimhakikishie tu kwamba tutafanya tathimini na kuona idadi ya wananchi kama inakidhi vigezo na umbali, na ikiwa itakidhi vigezo kata hiyo itakuwa ya kimkakati rasmi na tutatafuta fedha kwa awamu kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo hicho. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kituo cha Afya cha Ilula ambapo ni mji ndogo wenye idadi kubwa ya watu, kina majengo mengi sana ambayo hayajakamilika na kwa hiyo huduma zinazotolewa hazijakamilika. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kukamilisha majengo ya Kituo cha Afya cha Ilula? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Ilula kilipelekewa fedha, lakini bado kuna majengo ambayo hayajakamilika na hivyo, hakitoi huduma ile inayotakiwa. Kwa bahati nzuri nimeshawasiliana na Mheshimiwa Nyamoga na tumekubaliana kuwa tumeingiza kituo hicho kwenye mpango wa fedha wa Benki ya Dunia, kwa ajili ya kwenda kujenga majengo yale yaliyosalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Ilula kwamba wakati wowote kwanzia sasa fedha zitapelekwa, kwa ajili ya kuboresha miundombinu ambayo haijakamilika katika Kituo cha Afya cha Ilula. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Festo Richard Sanga, kwa niaba Mheshimiwa Kilave.

Na. 513

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Matamba, Makete**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE K.n.y. MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Matamba - Makete?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025 Serikali imetenga fedha ya nyongeza shilingi bilioni 53.5 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika kata 214 za kimkakati kwenye majimbo yote nchini. Awamu ya kwanza imeanza na ujenzi wa vituo vya afya katika kata 120, ambapo shilingi bilioni 30 zimetengwa na fedha hizi tayari zimeanza kupelekwa majimboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Makete, shilingi milioni 250 awamu ya pili zitapelekwa katika Kata ya Matamba kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa awamu, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika kata za kimkakati kote nchini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini je, tuna uhakika gani wa kupelekewa hizi fedha kwa sababu zile za mwanzo zilichelewa; je, hizi zitafika kwa wakati? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tunavyo vituo vya afya vya kimkakati ndani ya Jimbo la Temeke; je, fedha hizi ambazo wanasema zinaletwa ndani ya Jimbo la Temeke katika vituo vyetu vya afya viwili; cha Sandali pamoja na kile cha Temeke 14; ziko tayari kuletwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka minne tayari imekwishapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya zaidi ya 400 na hivi sasa katika bajeti ya nyongeza ya shilingi bilioni 53.5, tayari Serikali imekwishapeleka bilioni 30 na majimbo 120 kwenye kata za kimkakati ambazo zilianishwa Waheshimiwa Wabunge tayari wamekwishapokea fedha hizo na machache fedha zinaendelea kuingia.

Kwa hiyo ninaomba nimhakikishie, kwa mtiririko huu ni dhahiri kwamba tuna uhakika kwamba kata hizo nyingine ambazo zinasalia katika majimbo hayo zitapelekewa fedha pia kwa ajili ya kujenga vituo hivyo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, tunafahamu kwamba katika Jimbo la Temeke vipo vituo vya afya ambavyo Mheshimiwa Dorothy Kilave aliviainisha na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI na tayari tumeviingiza kwenye mpango kwa ajili ya kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi. Hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Temeke kwamba Serikali itapeleka fedha na kujenga vituo hivyo vya afya kwa awamu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, pale Halmashauri ya Mji wa Njombe tuna Kituo cha Kibena kikongwe na cha muda mrefu, tumeahidiwa mara nyingi; je, ni lini sasa fedha zitapelekwa kwenye kituo hicho?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Kibena katika Jimbo la Njombe Mjini ni kituo cha afya kikongwe na kichakavu, lakini pia kina upungufu wa miundombinu na Mheshimiwa Mbunge Deo Mwanyika, amefuatilia mara kadhaa. Tumekwisha kiingiza miongoni mwa vituo vya afya vikongwe vya kimkakati 203 ambavyo tutavitengea fedha. Mara baada ya kukamilisha ukarabati wa hospitali kongwe 53 tutahakikisha Kituo cha Afya cha Kibena kinapewa kipaumbele na kupelekewa fedha kwa ajili ya ukarabati na kuongeza majengo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kituo cha Afya Chuo Kikuu cha Mkwawa kinahudumia

wananchi wengi; je, nacho kinaweza kuingizwa kwenye vituo vya afya vya kimkakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha afya katika Chuo Kikuu cha Mkwawa tayari kimekwishaingizwa kwenye mpango wa upanuzi. Nimhakikishie Mheshimiwa Jesca Msambatavangu na wananchi wa Chuo Kikuu cha Mkwawa na wananchi wa jirani wanaopata huduma hizo kwamba tayari tunaendelea na utaratibu wa kutafuta fedha na tutakwenda kujenga majengo pale ili kituo kile kihudumie wananchi wengi zaidi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Tarime Vijijini na halmashauri yake wana mapato makubwa, Serikali ipo tayari kutoa mwongozo katika halmashauri zenye mapato makubwa Tanzania ili kupunguza mzigo wa Serikali, ili kila watakapopanga bajeti ya halmashauri hiyo waingize vituo vya afya katika maeneo hayo ili tujenge vituo vya afya. Walipotoa mwongozo ule tulijenga vituo vya afya viwili kwa mapato ya ndani. Sasa maeneo kama kule Gorong'a, Itiryo, Mkerege, Kiore, wanaweza kujenga vituo vya afya.

Je, Serikali ipo tayari kupeleka mwongozo wa maandishi kwamba kila bajeti ijayo inayokuja kwenye Bunge hili, halmashauri ambayo ina mapato makubwa itenge fedha kujenga kituo cha afya kimoja au viwili na zahanati? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kila mwaka wa bajeti Serikali huwa inatoa mwongozo wa bajeti na kila mwaka wa fedha tunaelekeza halmashauri kutenga kiasi cha fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa mfano kuna halmashauri ambazo zina mapato

chini ya bilioni tatu, zinatenga 40% ya fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kuna halmashauri ambazo zina mapato zaidi ya bilioni tano, zinatenga angalau 60% ya fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Vilevile ziko halmashauri zenye mapato makubwa zaidi zinatenga hadi 70% ya fedha zao za mapato ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na miradi hii ya maendeleo ni pamoja na sekta ya afya, kwa maana ya ukamilishaji wa maboma, ujenzi wa vituo vya afya, ukamilishaji wa maboma ya madarasa, shule na miradi mingine ya maendeleo.

Kwa hiyo, kama mwongozo tayari unatolewa kila mwaka na fedha zimewekewa kabisa maelekezo ya kutengwa kwa ajili ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuwakumbusha na kuwasisitiza Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kuzingatia vipaumbele. Zipo halmashauri zina vipaumbele vikubwa zaidi vya vituo vya afya; zipo nyingine zina vipaumbele vingine. Kwa hiyo lazima kila halmashauri kulingana na mahitaji, na Baraza la Madiwani lihusike kuainisha mahitaji kama ni vituo vya afya wahakikishe ile 40% au 60% au 70% inakwenda kujenga vituo vya afya ama miradi ambayo ni kipaumbele.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara hiyohiyo. Mheshimiwa Kapufi.

Na. 514

**Majengo ya Halmashauri ya Manispaa ya Tanganyika Ndani ya Manispaa ya Mpanda**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza: -

Je, kwa nini majengo ya Halmashauri ya Tanganyika yaliyopo ndani ya Manispaa ya Mpanda yasikabidhiwe kwa Halmashauri ya Manispaa Mpanda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ni halmashauri mama ya halmashauri zote za Mkoa wa Katavi ikiwemo Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda. Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika iligawana mali na madeni mwaka 2007 ilipoanzishwa Halmashauri ya Mji wa Mpanda (kwa sasa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda). Mgawanyo uliridhiwa katika Mikutano ya Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri za Mji wa Mpanda na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda (kwa sasa Tanganyika) kisha kusainiwa na halmashauri zote mbili na taarifa iliwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa barua ya tarehe 14/04/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 ya Mwaka 1982 katika vifungu namba 114 na 115 inazipa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ngazi za Wilaya fursa na uwezo wa kumiliki na kuendesha vitegauchumi katika eneo lolote ndani na nje ya mipaka yake. Hivyo, uwepo wa baadhi ya majengo yanayomilikiwa na Halmashauri ya Tanganyika ndani ya Manispaa ya Mpanda ni halali na imezingatia misingi ya kisheria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, leo hii ukija Mpanda majengo mbalimbali, ofisi, nyumba za watumishi zote zinamilikiwa na Halmashauri ya Tanganyika. Swali langu; je, ni kwa nini Serikali isiliangalie suala hili ukizingatia Manispaa ya Mpanda ina uhaba mkubwa mno wa nyumba za watumishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, lengo la Serikali kuanzisha mamlaka hizi mbalimbali ni kusogeza huduma. Mazingira yaliyofanya uanzishaji wa Halmashauri ya Tanganyika kwa kipindi kile ilikuwa ni halmashauri moja ya Mpanda; leo mazingira yamebadilika. Serikali akiwa ni mlezi wa mamlaka hizi mbalimbali; je, kwa nini asiangalie mazingira ya kuona tunawasaidiaje Manispaa ya Mpanda kwa wakati huu wa sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa ugawaji wa mali kati ya halmashauri mama na halmashauri mpya inayozaliwa, kwanza unafanywa kwa makubaliano ya Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri zote mbili. Hili ni jambo la msingi, kwa sababu ni ugawaji wa mali na madeni shirikishi ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ngoja. Waheshimiwa kuna Mjumbe anapiga simu humu ndani hampokei, kuna simu ya Mjumbe hiyo? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo ninaelewa hoja ya Mheshimiwa Kapufi kwamba yapo majengo, ziko nyumba za watumishi ambazo awali zilikuwa za Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda. Katika mgawanyo wao wa 2007 zilibaki halmashauri nyingine kwa maana ya Tanganyika, lakini ziko kwenye ardhi ya Manispaa ya Mpanda. Sasa tunafahamu hoja hiyo na mwongozo unaelekeza ofisi zibaki kwenye halmashauri pale zilipo, lakini majengo mengine yanaweza yakamilikiwa na halmashauri yoyote.

Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunaipokea hoja ya Mheshimiwa Kapufi, tukaifanyie tathmini na kuona, lakini pia tutakwenda kushirikisha pia Mabaraza ili tuwe na maamuzi shirikishi na kuona namna nzuri zaidi ya kuli-*manage* jambo hili na kulipeleka katika hatua nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Serikali inafahamu kwamba kuanzisha mamlaka mpya ni kusogeza huduma za kijamii karibu zaidi na wananchi na inaendelea kufanya hivyo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kufanya hivyo kuisaidia Manispaa ya Mpanda pale ambapo itahitajika ili iweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi wa halmashauri hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, *situation* kama iliyopo Manispaa ya Mpanda, Halmashauri ya Mji wa Tarime na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, mabaraza yalikaa yakaamua hivyo, lakini kwa sasa hivi, majengo yameshajengwa, ofisi na nyumba za watumishi na bado Halmashauri ya Mji wa Tarime ina uhaba wa nyumba za watumishi.

Je, Serikali haioni kwamba, kwa sababu imeshajenga kule, kuliko hata kuingia gharama mara mbilimbili, wakabidhi Halmashauri ya Mji wa Tarime zile nyumba za watumishi waweze kuzitumia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii ni hoja ya msingi, lakini kwa mujibu wa mwongozo na utaratibu, Mabaraza yalishiriki na yakafanya mgawanyo huo. Sisi kama Serikali tunalichukua hilo, tukalitazame katika utaratibu wa kutatua changamoto hiyo, lakini pia kuona katika *future plans* ni namna gani tutakuwa tunafanya katika kugawa miradi hiyo kwa halmashauri mama na halmashauri inayozaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tutalichukua hilo na tulifanyie tathmini na tuweze kuona namna gani tunaweza tukalifanya. Lakini ikumbukwe kwamba, mgawanyo wa mali na madeni ni shirikishi, mabaraza ya madiwani ya pande zote yanashiriki na Mwenyekiti wa Kamati hiyo ni Katibu Tawala wa Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakwenda kulifanyia kazi, lakini tutaona namna nzuri ya kuli-*manage*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Subira Mwaifunga.

Na. 515

**Kuwaandaa Wananchi Kutumia Nishati Safi ya Kupikia**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kuwaandaa wananchi kutoka kwenye nishati ya kupikia waliyoizoea kuingia kwenye nishati safi ya kupikia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwaandaa wananchi kutoka kwenye nishati ya kupikia waliyoizoea na kuingia kwenye nishati safi ya kupikia, Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanzisha mikakati mbalimbali ya uhamasishaji na utoaji wa elimu wa masuala ya nishati safi ya kupikia. Aidha, tarehe 2 Juni, 2025 Wizara ya Nishati imezindua Mkakati wa Mawasiliano wa Nishati Safi ya Kupikia unaotoa mwongozo wa kampeni zote zitakazofanyika kwa kushirikisha wadau mbalimbali, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati iliyopo Serikalini bado haijawafikia vilivyo wananchi hususani kwenye maeneo yetu. Nilitaka kufahamu na ndilo swali langu la msingi; nini Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba inawafikia Watanzania ambao tunataka watue nishati hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; Wabunge ni sehemu ya wahamasishaji wakubwa katika suala zima la nishati safi kwa wananchi wetu, je, Serikali haioni kwamba sasa umefika wakati wa kuwashirikisha Wabunge kikamilifu katika suala zima la nishati safi, ili kuweza kuwa na ufanisi kwenye maeneo yetu kuliko ilivyo hivi sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninashukuru kwa maswali mazuri ya Mheshimiwa Mbunge na nimpongeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la kwanza la mikakati ambayo Serikali inayo; la kwanza ni kuhakikisha tunaleta afua za kikodi kwa ajili ya kupunguza bei, lakini vilevile kwa ajili ya kuongeza matumizi kwa watumiaji wa kwanza. Changamoto kubwa ambayo tunayo kwenye masuala ya nishati safi ni kumfanya mwananchi aanze matumizi ya kwanza, kwa sababu vifaa vile vya matumizi kidogo ni gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa mwaka huu tayari tumeshafanya mazungumzo na wenzetu wa Wizara ya Fedha na kukubaliana baadhi ya maeneo ambayo tunaweza tukaanza kupunguza kodi, kwa ajili ya kumrahisishia mwananchi aweze kuwa na *access* bei, lakini vilevile tuweze kuanza matumizi ya kwanza kwa wale ambao bado hawajaanza matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali inaendelea kutoa ruzuku katika vifaa vya matumizi. Kama ambavyo mnaona karibia nusu bei kwa mitungi takribani 420,000 na ni mwanzo tu, tutaendelea kufanya hivyo. Vilevile tunahamasisha ubunifu mbalimbali kulingana na maeneo husika na teknolojia ambazo zinaweza zikatumika kwenye maeneo husika.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina mikakati mbalimbali na kwa kweli ajenda hii imebebwa kwenye moyo wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na sisi kama wasaidizi wake tunahakikisha tunalifanyia kazi ili tuweze kufikia 75% kwa mwaka 2030 na 80% kwa mwaka 2032. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kuwashirikisha Wabunge, kwa kweli na sisi tunatambua mchango mkubwa wa Wabunge katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, tulianza kufanya hivyo tangu kampeni hii inaanza. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Wabunge ni wadau wetu wa muhimu sana

tutaendelea kushirikiana nao katika kusukuma ajenda hii ya nishati safi ya kupikia, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Gulamali.

Na. 516

**Gharama Kubwa za Kuvuta Umeme Vijiji vya Manonga**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali inatoza gharama kubwa za kuvuta umeme Vijiji vya Chomachankola, Simbo, Nkinga Ziba na Iborogero – Manonga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetofautisha gharama za kuunganisha umeme kulingana na eneo husika, ambapo kwa maeneo ya vijijini gharama za kuunganisha umeme ni shilingi 27,000 na kwa maeneo ya mijini yakijumuisha makuu ya tarafa, makao makuu ya kata na maeneo ya vijiji miji wanalipia shilingi 320,960. Vijiji vya Chomachankola, Simbo, Nkinga, Ziba na Iborogero vinapatikana katika maeneo ya makao makuu ya kata, hivyo wateja wa maeneo hayo wanalipia shilingi 320,960 kama gharama ya kuunganisha umeme, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Nilikuwa ninapenda, ndiyo maana nimeuliza swali kumwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa sababu haya maeneo niliyoyataja ni maeneo ya vijijini. Hivyo basi kuona ni kwa namna gani Serikali inaweza ikapunguza gharama ili kuweza kuwarahisishia wananchi kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lapilli; sisi katika Jimbo letu la Manonga ni majimbo ya vijijini, tulikuwa tunahitaji umeme wa *REA* uweze kuongezwa katika maeneo ya vitongoji hasa katika Jimbo la Manonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaomba nijibu haya maswali mawili kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kweli kwa mara nyingi sana amekuwa akiniambia kuhusiana na maeneo haya na nimpongeze kwa kazi nzuri anayoifanya kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na maeneo ya kupunguza gharama, kwa Jimbo la Manonga pekee yake Serikali kwa kweli iliona ukubwa jimbo hili na namna ambavyo vitongoji vingi havina umeme katika jimbo hili na ndiyo maana katika mradi huu ambao sasa hivi tunatafuta wakandarasi tumempatia Mheshimiwa Mbunge vitongoji 86 ili wananchi wake waweze kunufaika na suala la uunganishaji wa umeme. Sasa kutokana na bei, wakati tunafanya miradi hii yaa vitongoji vijijini, wananchi wataunganisha umeme kwa shilingi 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwahamasisha wananchi wake, wakati miradi hii inaendelea basi waweze kuunganisha umeme kwa gharama ile ambayo inaunganishiwa umeme, ya shilingi 27,000; kwa sababu ndiyo gharama ambayo kwa kweli inaunganishwa wakati miradi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imejidhatiti kuendelea kupeleka umeme katika vitongoji na kwa kweli kama yeye anavyoona katika jimbo lake kwa kweli tumeangalia ukubwa wa

jimbo ndiyo maana amepata vitongoji 86. Nimhakikishie kwamba wakandarasi wanaokuja watakuwa ni wazuri sana na miradi hii itaenda kwa kasi na wananchi wake wa Manonga wataendelea kunifaika na suala la umeme.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo gharama za kuunganisha umeme za shilingi 27,000 zinazotajwa hapa, ukienda kule kwa wananchi uhalisia wakiandika barua kuomba maombi wanaletewa gharama tofauti kabisa na hiki ambacho kinasemwa hapa; na imekuwa ikiwachanganya sana wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata haya makao makuu ya tarafa wanayosema kwamba itaunganishwa kwa gharama ya shilingi 320,000 makao makuu yetu ya tarafa ni vijiji, hizo gharama ni kubwa sana. Kwa nini Serikali isifikirie, kwa sababu ghamara zote za kimiundombinu zinabebwa na Serikali kwa 100%; lakini kwenye kuunganisha tu mnamtaka mwananchi abebe gharama hizo kwa kazi ya shilingi 320,000 au shilingi 27,000; ni hela nyingi sana. Kwa nini msifikirie ku-*review* hizi *price* ili wananchi wengi zaidi wavute umeme kwa gharama nafuu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninashukuru kwa maswali mazuri ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya kuunganisha umeme ni shilingi 27,000 na hii ni gharama ambayo mwananchi atakuwa haitaji nguzo kwenye kuunganisha umeme, lakini sasa ikishafika suala la nguzo ndipo hapo tunaposema gharama yake inatofautishwa. Kwa sababu kuunganisha umeme kunategemea na umbali wa anayeunganishiwa kutoka kwenye chanzo cha

umeme huo. Kwa hiyo, sasa gharama *flat* kabisa kama ambavyo mwananchi haitaji nguzo au chochote, gharama ni shilingi 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Serikali tunaendelea kupeleka umeme kwenye vitongoji, kwa ajili ya kupunguza umbali ule ambao mwananchi anaambiwa alipie nguzo kwa ajili ya kumfikia. Kwa hiyo, sasa kwa miradi ambayo inaendelea ya vitongoji tutapunguza umbali na hata gharama kwa wananchi katika kuunganisha umeme. Kwa hiyo, sasa hivi tunaona changamoto kwa sababu umeme umefika kwenye makao makuu ya kijiji, haujafika ndani kwenye vitongoji. Kwa hiyo, tunavyoendeleza kupeleka miradi hii kwenye vitongoji ndivyo ambavyo tunamsaidia mwananchi kupunguza gharama na yeye aweze kuwa na *access* kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu Serikali imejidhatiti na imeji-*commit* kuendelea kufikisha umeme kwenye vitongoji, tuvute subira tutaweza kuona tu namna ambavyo tunaleta unafuu kwa wananchi kupitia miraadi hii ya vitongoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la kupunguza bei. Waheshimiwa Wabunge, ninyi mnafahamu sasa hivi katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, tumeweka mkakati wa kupeleka umeme kwenye vitongoji. Kwa hiyo, kwa sababu mikakati ni mingi na sisi tunataka kwanza turahisishe *access,* halafu bei ifuate basi tuendelee kuvumilia, tuwape kwanza wananchi *access* na suala la bei tutaendelea kufanyia kazi taratibu taratibu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MKAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, wananchi wa Kijiji cha Mahanje katika Kata ya Mahanje Kitongoji cha Kipera, wamekuwa na malalamiko makubwa kutokana na ucheleweshwaji wa ukamilishaji wa mradi wa usambazaji wa umeme kwenye Kitongoji hiki cha Kipera.

Je, ni lini sasa Serikali itakuwa tayari kuhakikisha kwamba mkandarasi anakamilisha ule mradi kama ambavyo imekusudiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kijiji hiki cha Mahanje, Kitongoji cha Kipera, kwa kweli nitafuatilia nikitoka hapa nijue changamoto aliyonayo mkandarasi ili tuweze kuitatua, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa wakandarasi ambao tumewapatia kazi kwa kweli hatukubaliani na suala la uchelewashaji wa uzembe katika kuwafikia wananchi umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutalitatua suala hili. Kama jambo lipo kwa mkandarasi na kama ana changamoto, basi tutawasiliana naye kuona ni namna gani tutatoa hizo changamoto ili wananchi wako hawa wa Kijiji cha Mahanje, Kitongoji cha Kipera waweze kumaliziwa mradi katika eneo hilo na wenyewe waweze kunufaika na suala la upatikanaji wa umeme katika Kitongoji hiki cha Kipera.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo; Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, kwa niaba ya Mheshimiwa Asha Abdullah Juma? Mheshimiwa Mayenga.

Na. 517

### Maji kwenye Mashamba ya Umwagiliaji Kufika Mashambani bila Upotevu

**MHE. LUCY T. MAYENGA K.n.y. MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha maji kwa ajili ya umwagiliaji yanafika mashambani bila upotevu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri. Kaeni kimya huko.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji nchini ili kuhakikisha wakulima wanapata maji ya uhakika mashambani na kuondoa upotevu wa maji kwa ajili ya umwagiliaji. Katika kutekeleza hilo, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji; ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya uhifadhi maji ili kuondoa upotevu wa maji wakati wa mvua; na kutoa elimu kwa wakulima juu ya matumizi sahihi ya maji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha hayo yanafanyika kikamilifu, Serikali imeamua kuwekeza kwa makusudi kwenye umwagiliaji kwa kuongeza bajeti ya maendeleo ya umwagiliaji kutoka shilingi bilioni 46.5 mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 331.8 mwaka 2024/2025 na kuongeza utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji kutoka 13 mwaka 2021/2022 hadi 780 mwaka 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mayenga.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali hasa kupitia Wizara ya Kilimo imefanya kazi kubwa sana kwenye miradi ya umwagiliaji hapa nchini; je, iko tayari sasa kuongeza kiwango cha miradi pamoja na pesa kwenye maeneo ambayo yana ukame ambayo yamethibitika kupata kiwango kidogo cha mvua kama Wilaya ya Kishapu ili kuweza kuwasaidia wakulima wengi zaidi na Watanzania wengi waweze kufaidika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nimpongeze Mheshimiwa Lucy Mayenga kwa kulifuatilia jambo hili na nimthibitishie tu kwamba kuongeza miradi hususani katika maeneo yenye ukame pamoja na fedha ni maelekezo ambayo tulishapewa na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ili kuhakikisha na yenyewe yanafanya kilimo cha uhakika. Kwa hiyo, katika Jimbo la Kishapu ambalo amelielezea ni sehemu

ya mpango wa Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Yahya Mhata.

Na. 518

**Hitaji la Chuo cha *VETA* – Nanyumbu**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha *VETA* Wilayani Nanyumbu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Nanyumbu ni miongoni mwa vyuo 64 vya *VETA* vinavyojengwa na Serikali katika Wilaya ambazo zilikuwa hazijajengewa vyuo vya ufundi stadi pamoja na chuo kimoja cha Mkoa wa Songwe ambao ulikuwa hauna Chuo cha *VETA* cha Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza ya ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Nanyumbu unatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 1.6 ambapo hadi sasa kiasi cha shilingi 682,881,780.24 kimetumika. Aidha, ujenzi wa chuo hiki umefikia 41% na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Chuo hiki cha *VETA* cha Wilaya ya Nanyumbu kilikuwa kikamilike mwezi Juni mwaka huu. Kulingana na majibu ya Serikali inaonekana sasa kitakamilika mwezi Novemba; je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Jimbo la Nanyumbu ambao walikuwa wamejipanga kuanza kukitumia chuo hiki mwezi Julai?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kulingana na awamu ya kwanza ya ujenzi wa Chuo cha *VETA* pale Wilayani Nanyumbu kulikuwa na majengo tisa na hadi sasa majengo sita ndiyo yanapauliwa, majengo matatu ambayo ni kwa ajili ya karakana yapo katika hatua ya msingi. Je, upo tayari kuwaambia wananchi wa jimbo langu kwamba mwezi Novemba pamoja na hizi karakana zitakuwa zimekwisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana kwa ufuatiliaji wa karibu wa ujenzi huu, lakini ninaomba nimhakikishie ni kweli kwanza tukiri mwanzoni tulikuwa na *commitment* ya kukamilisha miradi hii yote ya vyuo 64 vya wilaya na kile kimoja cha mkoa katika mwezi huu wa Juni, lakini kutokana na changamoto ya mtiririko wa fedha au tunaita *cash flow* imepelekea sasa tuweze kusogeza mbele kidogo kwa sababu tulichelewa kupata fedha ya awamu ya mwisho kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi huu. Hata hivyo, ninaomba nimhakikishie hivi sasa tayari tulishapokea zile shilingi bilioni 21.3 ambazo zilikuwa zimesalia kule Wizara ya Fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huu. Kwa hiyo, *target* yetu hivi sasa ya mwezi wa 11 kwa majengo haya itakuwa imefikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili amezungumzia zile karakana tatu ambazo tunajenga kwa kutumia Mfumo wa *Light Guage Steel* (*LGS)* kwa maana ukishamwaga lile jamvi hatua inayofuata ni kusimika zile nguzo za chuma na *infill* yake vilevile kwa maana zile kuta zitakuwa vilevile za mabati. Kwa hiyo,

ujenzi ule unachukua muda mfupi sana, lilikuwa suala la *mobilization* pamoja na kumlipa mzabuni ambaye tayari sasa ameshalipwa na sasa hivi tunafanya *delivery* ya hizo chuma pamoja na mabati ya kupaulia na kuezeka kwa ajili ya ujenzi wa hizo karakana; na utakamilika sambamba na majengo haya sita uliyokuwa umeyataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto iliyopo kwenye Jimbo la Nanyumbu ni sawa kabisa na Jimbo la Tunduru Kaskazini, ujenzi wa majengo ya awali ya Chuo cha *VETA* umesimama kwa muda mrefu sana. Tunataka kufahamu; je, ni lini ujenzi ule utaendelea na lini utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nikijibu swali dogo la Mheshimiwa Kungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishaeleza kwenye kesi ya Nanyumbu, inalingana na kesi ya Jimbo la Mheshimiwa Kungu. Ninaomba nikuthibitishie tu kwamba changamoto ilikuwa ni ileile ya *cash flow* kwa maana mtiririko wa fedha. Kama nilivyosema kwamba fedha sasa tumeshapata zilikuwa zimesalia shilingi bilioni 21 kwa ajili ya awamu ya mwisho ya ukamilishaji na hivi sasa ninaomba nikuthibitishie mbao zote, mabati yote na vyuma vyote tumeshalipia na tumeshanunua tayari kwa ajili ya ku-*deliver* kule *site*. Tunaamini tutakapofika mwezi Novemba majengo yale yote tisa yatakuwa tayari na itakapofika Januari sasa mafunzo yataanza kutolewa katika maeneo haya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Noah, ajiandae Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Katika Jimbo la Arumeru Magharibi kulikuwepo na maelekezo kwamba tungejengewa *VETA* ambayo tulionesha mpaka na eneo; je, ni lini sasa Serikali itaenda kujenga *VETA* katika Jimbo la Arumeru Magharibi katika maeneo yale ambayo tumeainisha ili kuwasaidia wananchi waweze kupata huduma hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nikijibu swali dogo la Mheshimiwa Saputu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani Mheshimiwa Saputu alikuja ofisini na tulikaa tukaongea kwa kina sana. Kimsingi katika Wilaya ya Arumeru kuna majimbo mawili ya uchaguzi, kwa hiyo, kimsingi *VETA* inajengwa katika jimbo moja na bahati nzuri katika jimbo linalojengwa siyo hili la Mheshimiwa Saputu na tulikubaliana Mheshimiwa Saputu katika majimbo yote ambayo yatakuwa hayana vyuo hivi vya *VETA* tutakwenda kujenga shule ya sekondari ya amali ndiyo mchakato na mtiririko unaoendelea hivi sasa. Tayari fedha hizo shilingi milioni 528 zimeshatengwa kwa ajili ya kupelekwa kwenye Jimbo la Mheshimiwa Saputu ambapo kule tutakwenda kujenga shule ya sekondari ya amali na lile jimbo lingine tunakwenda kujenga Chuo cha Ufundi *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ilipata kujengewa Chuo cha *VETA* mpaka sasa chuo hicho kimekwama takribani zaidi ya miezi nane; ni lini Serikali italeta fedha za kumalizia chuo hicho pamoja na *material*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Mheshimiwa Kakoso ni kweli ujenzi ulisimama kwa zaidi ya miezi nane, lakini ninaomba nikuthibitishie sasa kuwa tulishapata fedha, zilikuwa ni shilingi bilioni 43 ambazo tulikuwa hatujapata. Mwezi wa pili tulipata shilingi bilioni 20 na hivi wiki iliyopita tumepata shilingi bilioni 21 kwa hiyo inatengeneza jumla ya zile shilingi bilioni 40 na kitu ambazo tulikuwa bado hatujazipata, tumezitapa na tumeshapeleka fedha zaidi ya shilingi milioni 100 na kitu kwa ajili ya *local material* na *labor* kwa ajili ya kulipa wale mafundi na vifaa vipo njiani vinakwenda kule Tanganyika kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Chuo chetu cha *VETA* katika Wilaya ya Tanganyika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano, Mheshimiwa Felista Njau.

Na. 519

**Hitaji la Mnara wa Mawasiliano – Shimbwe**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga mnara wa mawasiliano katika Kata ya Shimbwe ambapo hakuna mawasiliano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* ilianisha Kata ya Shimbwe katika zabuni iliyotangazwa kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijiti mwaka wa fedha 2022/2023 na utekelezaji wake ulianza mnamo Mei 13, 2023 baada ya kumpata mtoa huduma Kampuni ya Honora *(YAS)*. Ujenzi wa mnara huu kwa sasa umekamilika, ni imani yetu kukamilika kwa mnara katika kata hii, kumeimarisha hali ya mawasiliano na endapo changamoto zaidi zitabainika kuendelea kuwepo katika Kata hii ya Shimbwe, basi nitaielekeza *UCSAF* kufanya tathmini ya namna bora ya kuzitatua.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, kwanza niishukuru Serikali kwa namna ambavyo ililichukulia hili suala niliuliza katika swali la nyongeza na wamechukua hatua. Ninaishukuru Serikali kwa kuchukua hatua, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kata ya Shimbwe kuna Kata za Kimochi, Kibosho Mashariki na Uru Kaskazini ambazo hazina minara kabisa, ni lini Serikali itajenga minara hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, wanakwenda na *YAS* lakini wananchi wengi wa Moshi Vijijini wanatumia mitandao mbalimbali. Sehemu ambazo zina minara bado mawasiliano ni magumu kabisa na wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini wanapata shida ya mawasiliano nini makakati wa Serikali kuimarisha mawasiliano ili wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini waweze kupata huduma hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza nipokee shukrani zako kwa Serikali hakika Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni sikivu na lengo la Serikali ni kuhakikisha kata zote tunazifikia katika ujenzi wa minara na kuhakikisha mawasiliano yanakuwa bora kabisa. Nikupongeze na wewe na ufuatuliaji mzuri, lakini vilevile kata hizi nyingine ulizozitaja tutaendelea kujenga minara kadiri tunavyopata fedha na hasa katika mwaka ujao wa fedha kwa sababu sasa tayari tupo ukingoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, minara ya watoa huduma wengine nje ya *YAS* tutahakikisha tunaendelea kuwahimiza watoa huduma waweze pia kutumia minara ambayo tayari imejengwa ili kuokoa muda na gharama ili wakaweze kuweka vifaa vyao ili wananchi wapate kuchagua waweze kutumia watoa huduma gani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza na nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum - CHADEMA kwa swali lake ninamshukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, angekuwa na taarifa kamili kutoka kwa Mbunge wa Jimbo kwa miradi inayoendelea kwenye Jimbo langu la Moshi Vijijini labda ingemsaidia sana, kwa sababu ninasimama hapa ili niishukuru Serikali, imenipa minara minne ambayo imeshajengwa kwenye Jimbo langu la Moshi Vijijini ikiwemo hilo la Uru – Shimbwe. Kwa hiyo, ninaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la nyongeza, ninajua kilichobaki ni kuweka uzio kwa mfano kwenye ule Mnara la Uru – Shimbwe, tunawashukuru mmeshaujenga, kilichobaki ni kuweka uzio ndiyo taarifa niliyonayo kama Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo. Je, ni lini Serikali itajenga uzio ili kukamilisha mradi huu ambao ni wa kimkakati na tuliuomba na Serikali ilinisikiliza? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kwa ufuatiliaji, juzi ulipokuja Wizarani hili tulishaliweka sawa, lakini suala la uzio kama ulivyoahidiwa na Mheshimiwa Waziri na watoa huduma wote wamekuwa wakisisitizwa lazima waweke uzio kwa sababu fedha inayotumika kuwekeza katika hii minara ni nyingi, kwa hiyo lazima tulinde mali za Serikali pamoja na fedha za wananchi kwa sababu fedha hizi zinapatikana kutokana na kulipa kodi. Kwa hiyo, nikutoe hofu uzio tunakwenda kuujenga. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante, Mheshimiwa Waziri kuna baadhi ya minara inakuwa mbali sana na mnara inayofuatana na hii inafanywa sababu wanaohusika na kampuni hizi kupunguza gharama ya kuongeza minara wanaweka minara inakuwa mbali sana. Tatizo linakuja lazima waongeze *frequency* ya kupeleka mawasiliano kwenye mnara ambao upo mbali, *doing* so wana-*create emission* ya *radiation*.

Je, minara hii ina *radiation,* mnapima ina viwango ambavyo vinakubalika kutokuathiri maisha na afya za watu? Lipokee huu ni ushauri tu wala usilijibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa *Engineer* Ezra.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, niishukuru Serikali kwa minara iliyonipatia Biharamulo ni mingi kwenye baadhi ya maeneo, lakini nilileta maombi pia kwa sababu kuna maeneo kama Kata ya Nyamigogo ina vijiji vinne hakuna mnara hata mmoja lakini baadhi ya maeneo ya Kata ya Lusahunga, Kata ya Kaniha, Katahoka, Runasi, Nemba na Nyakahura. Sasa ni lini Serikali itafanyia kazi maombi haya ili kata zote 17 za Biharamulo ziwe katika mawasiliano *full* ili mtu anayetoka eneo moja kwenda eneo lingine asifike sehemu mawasiliano yakakatika? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Nikupongeze Mheshimiwa *Engineer* Ezra kwa ufuatiliaji lakini vilevile kama ulivyoweza kushuhudia mwenyewe minara mingine kujengwa katika maeneo yako, kata hizi chache ulizozitaja kama ulivyoleta maombi lazima tuje tufanyie kazi mwaka ujao wa fedha tutahakikisha tunaanza kata moja baada ya nyingine ili kuhakikisha wananchi wote wanaweza kunufaika na mawasiliano ya uhakika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano ni kitu muhimu sana katika karne hii. Sasa pale Makambako kutoka Makambako kwenda Njombe pale Lyamkena na Kiumba tumejenga soko kwa ajili ya biashara za nchi jirani ya mazao, mawasiliano hakuna ni

kilometa nne tu kutoka mjini kwenda hapo, na kutoka Makambako kwenda Mbeya pale Majengo ni kilometa tatu hakuna mawasiliano kwa mjini. Je, Serikali iko tayari kuhakikisha inaweka *booster* kwa ajili ya mawasiliano katika maeneo mawili haya niliyoyataja? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nikupongeze sana Mheshimiwa Deo Sanga kwa ufuatiliaji wa maeneo haya kuhakikisha mawasiliano yanaimarika. Lengo la Serikali kwenye barabara kuu zote ni mawasiliano yaweze kupatikana toka *entry* A mpaka Z. Kwa hiyo, tuko katika mkakati wa kuhakikisha maeneo yote ambayo hayana mawasiliano kwenye barabara kuu zetu yanapata mawasiliano. Nikupe tu uhakika sisi kama Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari tuko tayari kuhakikisha kwamba tunakuja kufanyia kazi maeneo haya uliyoyataja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, Kata ya Ngofila ina changamoto ya mawasiliano na bahati nzuri *TTCL* wameingia mkataba kwa ajili ya ujenzi wa mnara katika Kata ya Ngofila. Je, Serikali ipo tayari kuweka msukumo ili mkandarasi aanze kutekeleza mradi huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Butondo kuwa kata aliyoitaja *TTCL* lazima waje wafanye kazi. Kwa kupitia Bunge lako Tukufu, ninaomba niagize *TTCL* ambaye amepewa hii kazi waende kufanya mara moja kadri ya mkataba ulivyosainiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, Serikali ilituahidi kuimarisha mawasiliano kwenye

Kata ya Ovada, Lalta pamoja na Lahoda kwa kupeleka watoa huduma wengine.

Je, ni lini sasa Serikali mtatuongezea ama mtapeleka hao watoa huduma wengine ili mawasiliano kwenye kata hizi yaweze kuimarika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kumpongeza Mheshimiwa Kunti Majala kwa ufuatiliaji, watoa huduma wengine tayari tumeshaagiza kwamba waje wahakikishe wanatumia minara iliyopo, wanajua namna ya kufanya mawasiliano na wenzao waliyotangulia ujenzi wa mnara kuokoa muda na gharama, lengo ni mwananchi apate aina zote za mitandao ili iwe rahisi kwa mawasiliano yao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Koka.

Na. 520

**Ujenzi wa Barabara ya Makofia – Mlandizi – Vikumburu**

**MHE. SYLVESTRY F. KOKA** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa kiwango cha lami wa Barabara ya Makofia – Mlandizi – Vikumburu utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Barabara ya Makofia – Mlandizi – Vikumburu unafanyika kwa awamu ya kwanza ya sehemu ya Mlandizi hadi Makutano ya Stesheni ya *SGR* ya Ruvu (kilometa15) mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 2 Mei, 2025. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi eneo la Mji Mdogo wa Mzenga ambao pia utahusisha uwekaji wa taa. Kwa sehemu

iliyobaki ujenzi utaendelea kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Koka.

**MHE. SYLVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na kazi nzuri ya Serikali inayoenda kuifanya nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya njia nane kutoka Dar es Salaam hadi Kibaha imesababisha msongamano mkubwa sana wa magari kwa Barabara ya Morogoro kuanzia pale Kibaha Mjini kwa maana ya Maili Moja, kwa Mathias, Kongowe, Visiga hadi Chalinze.

Mheshimiwa Naibu Spika, baya zaidi magari makubwa sasa yameanza kuchepuka na kuingia katikati ya Mji wa Kibaha yakiharibu barabara za lami zilizo katika mji huu wa Kibaha.

Je, ni lini sasa barabara ya njia nane itaanza kujengwa kuanzia Kibaha hadi Chalinze kama Serikali ilivyoahidi?

Swali la pili, Barabara ya Tamco hadi Mapinga yenye urefu wa kilometa 23 imejengwa kwa kusuasua sana ni takribani ya zaidi ya miaka saba ni kilometa kumi tu ndiyo zimejengwa. Je, ni lini Serikali itakamilisha barabara hii muhimu ili uchumi wa Kibaha Mjini uweze kuchangamka? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hapa tunapoongea mhandisi mshauri anafanya kazi ya kusanifu barabara pale tulipoishia njia nane ambapo tutajenga mpaka Picha ya Ndege kilometa 3.8 kwa hizo njia nane na mhandisi mshauri yuko *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia pale Picha ya Ndege kwenda Mlandizi, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea na majadiliano na wabia kwa maana ya sekta mbalimbali, Wizara yetu, Wizara ya Fedha na mbia ambaye atajenga siyo hizo njia nane, tunasema *express way* ambayo itajengwa kuanzia na kipande cha Picha ya Ndege hadi Mlandizi ambayo itakuwa ni mwendelezo wa kuja Morogoro. Kwa hiyo, tayari taratibu hizo zinaendelea tuko kwenye majadiliano na watu ambao tunategemea waje watujengee *express way*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Barabara ya Tamco - Mapinga, nikubaliane naye, lakini atafahamu kwamba kulikuwa na changamoto ya fidia. Tunapoongea mkandarasi amesharejea *site* na Serikali imeshalipa fidia yote ambayo ilikuwa inakwamisha tuweze kushindwa kuendelea kujenga. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunakwenda kukamilisha, tumeshalipa fidia na mkandarasi amesharudi *site*. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza kuhusu ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami ya Morogoro – Mlimba – Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, juzi kipande cha kutoka Ifakara - Mbingu - Igima tayari mkandarasi ameweka bango akiashiria anaanza kazi.

Swali langu dogo la nyongeza, je, ni lini mkandarasi wa kipande cha kutoka pale Mbingu - Igima kwenda Chita atakabidhiwa kazi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Rais tupokee pongezi za Mheshimiwa Mbunge wa Mlimba, lakini kuhusu kipande alichokiuliza kuanzia

Mbinga kwenda Chita tulishasaini mkataba na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi tunachosubiri na wenzetu wa Wizara ya Fedha wametuhakikishia kwamba sasa na sisi tumeshaanza kupokea fedha kutoka Wizara ya Fedha kwa maana ya zile hati za malipo, lakini pia malipo ya awali. Kwa hiyo, tukishamlipa malipo ya awali mkandarasi huyo ataanza kazi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Wambura.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, barabara ya kutoka Mkunwa ambapo ni makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara kwenda katika Hospitali ya Wilaya ya Nanguruwe imejengwa kwa kiwango cha lami kwa kilometa 3.8 kwa muda wa miaka miwili. Je, ni lini kilometa zote 17.5 zitajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, tumeshaanza kujenga hizo kilometa 3.8 lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tunajenga kwa awamu kadiri fedha inapopatikana tutahakikisha tunakamilisha kipande chote cha hizo kilometa ambazo zimeshasanifiwa kwa ajili ya kuzijenga zote, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyoka.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya kutoka Mulete, Making'inda, Mkuzo hadi Mwenge Mshindo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, swali fupi nawe jibu kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilisha usanifu wa hiyo barabara tutaanza kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ningependa kufahamu majadiliano kati ya mkandarasi anayetarajiwa kupewa kazi ya ujenzi wa barabara ya kutoka Mwanza kwenda Usagara kwa njia nne imefikia wapi ili mkandarasi akabidhiwe kazi na kuanza mara moja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, majadiliano yako kwenye hatua za mwisho ambapo tunajaribu kuangalia asije akaanza kujenga kwa gharama kubwa. Kwa hiyo, ni kazi ya Serikali kuhakikisha kwamba wanafanya majadiliano ili aweze kuwa kwenye bei ambazo tunajua ndizo bei za soko kwa sasa. Kwa hiyo, kazi inaendelea na itakapokamilika tutamjulisha Mheshimiwa Mbunge, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa lami kilometa moja Mjini Mwanhuzi ikiwa ni pamoja na kuweka taa na kumlipa mkandarasi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ni kweli katika miji yote ambako barabara za *TANROADS* zinapita kwenye miji huwa tunaweka lami na taa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakamilisha katika bajeti inakuja na tumeweka fedha kwa ajili ya kukamilisha hicho kipande ikiwa ni pamoja na kuweka taa katika Mji wa Mwanhuzi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Subira.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa kuipandisha hadhi Varabara ya Mingoi - Kiembeni kwenye Kata ya Mapinga kama ambavyo imeahidi hapa Bungeni? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za kisheria zikisha kamilika kwa maana ya wataalam kwenda kufanya tathmini na kutoa ripoti kwamba barabara hiyo inapanda hadhi Wizara ya Ujenzi itaichukua hiyo barabara ilimradi tu iwe imekidhi vigezo vyote vya kuipandisha barabara kutoka *TARURA* kuja *TANROADS*, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara kutoka Kongwa kwenda Mpwapwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo barabara iko kwenye mipango, atakubaliana nami kwamba ni barabara ambayo tayari ilishapata mkandarasi na kinachosubiriwa ni kulipwa *advance* mkandarasi huyo ili aweze kuanza kujenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mageni.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, barabara inayotokea Bujingwa kupitia Kolomije - Mantare mpaka Malya ni barabara muhimu sana kwenye uchumi wa Jimbo la Sumve, lakini barabara hii haijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu na juhudi za kuwasiliana na *TANROADS* ili ukarabati ufanyike tumezifanya lakini hakuna kilichofanyika. Je, nini tamko la Wizara kuhusu ukarabati wa barabara hii ili iweze kupitika muda wote?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge amefika ofsini kuhusu hiyo

barabara na tumeshamwelekeza Meneja wa Mkoa wa Mwanza wa *TANROADS* kwamba kwa kuwa mkandarasi yupo na mvua sasa haipo arudi barabarani ili aweze kuhakikisha kwamba anaikarabati hiyo barabara na inapitika muda kuanzia sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumwelekeza tena Meneja wa Mkoa wa Mwanza ahakikishie mkandarasi ambaye yuko *site* aanze hiyo kazi ya kukarabati barabara, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Naibu Waziri, mkumbushe tena Meneja wako wa Dar es Salaam, lile eneo la Jangwani kuelekea Klabu ya Yanga maelekezo yako mpaka leo bado hawajatekeleza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Wageni waliyopo Bungeni asubuhi hii.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu; wageni wawili Ndugu Ibrahim Ndolo, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ruangwa, karibu. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Salumu Titili Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Liwale, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika; wageni watatu wa Mheshimiwa Hamza Said Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Familia yake kutoka Jijini Dodoma; Ndugu Mwatunza Said, mama mzazi wa Mheshimiwa, karibu mama, umezaa chema na huyu ni mtu mwamba sana humu ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Ndugu Neema Johari, mke wa Mheshimiwa, karibu sana, mke wa Mheshimiwa *AG*. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Reefat Johari, mtoto wa Mheshimiwa, ahsanteni. *(Makofi)*

Tunao wageni 18 wa Bunge, Madaktari Bingwa wa Dkt. Samia wanaotoa huduma Bungeni kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete *(JKCI),* Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*, Taasisi ya Afya ya Akili Mirembe, Hospitali Maalum ya Magonjwa ambukizi Kibong'oto, Taasisi ya Mifupa Muhimbili *(MOI)* na Hospitali ya Benjamini Mkapa, karibuni sana mabingwa wetu mnaotoa huduma za afya nchini, hongereni sana kwa kazi nzuri mnazofanya. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni 75 wa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya *White Lake* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambao ni Kikundi cha Mwanamke Shujaa kutoka Rungwe, Mkoani Mbeya, karibuni. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mhandisi Ernest Martin, shemeji yake kutoka Mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, jamaa zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Sylivia Francis Sigula, makada wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Mkoani Iringa. *(Makofi)*

Tunao wageni 18 wa Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, wafanyabiashara, wakulima na wafugaji kutoka Wilaya ya Mlimba, Mkoani Morogoro wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, Ndugu Innocent Mwangasa. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo ambao ni jamaa zake kutoka Moshi, Mkoani Kilimanjaro, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni 17 wa Mheshimiwa George Malima ambao ni makada wa CCM kutoka Wilaya ya Mpwapwa, Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Samweli Hhayuma Xaday, Wachungaji na Wazee wa Makanisa ya *Pentecost, Assemblies of God* kutoka Hanang Mkoani Manyara, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 55 wa Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya, Kikundi cha Vijana cha *Pathfinder Club* kutoka Kanisa la Waadventista Wasabato Chang'ombe Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 33 na walimu watano wa Shule ya Awali na Msingi *JC Oghaban* kutoka Mkuranga, Mkoani Pwani, karibuni. Naona *uniform* yenu mmevaa ki-Scottish yaani, hongereni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 71 na walimu tisa wa Shule ya *St. Mary`s International School* kutoka Ifakara, Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *AG.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kabla ya kutoa hotuba kuhusu Muswada huu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge na kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu

kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa umahiri, mafanikio makubwa na uzalendo wa hali ya juu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila lenye kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe kama Naibu Spika, lakini na kumpongeza Spika wetu pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazoliongoza Bunge hili Tukufu. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuungana na Watanzania wenzangu pia kumpongeza pia Profesa Mohamed Yakub Janabi kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika katika Shirika la Afya Duniani na kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania katika tasnia ya afya ulimwenguni. Ninamtakia kheri katika majukumu yake mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninaishukuru sana Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama - Mbunge na Makamu wake Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo – Mbunge, pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua muswada huu kwa umakini na kuishauri Serikali kuboresha muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu uliotolewa na kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Afya na Wizara ya Uchukuzi na wadau wengine wote kwa ushirikiano waliotupatia katika mchakato mzima wa kushughulikia muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria pamoja na menejimenti yote na watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mchango wao mkubwa na msaada wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kipekee nichukue nafasi hii kumshukuru mama yangu mzazi Ndugu Mwatunza Said na mke wangu kipenzi Ndugu Neema Johari na watoto wangu Tamika Hamza Johari, Salita Hamza Johari na Rifath Hamza Johari kwa michango yao mbalimbali wanayonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025)* ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu leo, unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Tisa zifuatazo:-

(i) Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200;

(ii) Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sura ya 177;

(iii) Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182;

(iv) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413;

(v) Sheria ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Sura ya 150;

(vi) Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Sura ya 59;

(vii) Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268;

(viii) Sheria ya Bandari, Sura ya 166; na

(ix) Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317.

Mheshimiwa Naibu Spika, muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi. Sehemu ya kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la muswada na namna ambavyo sheria zinapendekezwa kurekebishwa katika sehemu zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200 ambapo kifungu cha 26 kinapendekezwa kufutwa. Marekebisho haya yanakusudia kuwezesha mashtaka chini ya sheria hii kufunguliwa bila kuhitaji ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwa la ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka kabla ya kufungua shitaka chini ya sheria hii liliwekwa miaka ya nyuma ambapo sehemu kubwa ya mashtaka yalikuwa yanaendeshwa na askari polisi kwa kuwa Ofisi ya Taifa ya

Mashtaka haikuwa imeenea katika mikoa na wilaya zote nchini. Hivyo, kulikuwa na umuhimu wa kupata ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka ili kudhibiti ufunguaji holela wa mashtaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira ya sasa ambapo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imefungua ofisi zake hadi ngazi ya Wilaya na kesi zote za jinai zinaendeshwa na Mawakili wa Serikali wanaowajibika moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, masharti ya kupata ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka yanakosa mantiki ya kuendelea kuwepo na yanaweza kuchangia ucheleweshaji wa haki jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ya muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sura ya 177. Kifungu cha tatu kinapendekezwa kurekebishwa ili kutafsiri upya msamiati "*chemical*" kwa kuwianisha tafsiri ya msamiati huo na tafsiri ya msamiati "*chemical*" iliyotolewa katika Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182. Lengo la marekebisho haya ni kutoa tafsiri itakayojumuisha masuala ya silaha za kikemikali yanayopendekezwa kuongezwa katika wigo wa Sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha saba kinapendekezwa kurekebishwa kwa kupunguza mwakilishi mmoja kutoka taasisi za elimu ya juu au taasisi za utafiti kama Mjumbe wa Bodi na kubaki na mwakilishi mmoja kutoka katika taasisi hizo kwa kuwa taasisi hizo tayari zina uwakilishi katika Kamati za Kitaalam, ikiwemo Kamati ya Kitaalam ya Usimamizi wa Kemikali, Kamati ya Kitaalam ya Udhibiti wa Vinasaba vya Binadamu na Kamati ya Kitaalam ya Kudhibiti Matukio ya Sumu ambazo kazi zake ni kuishauri Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile inapendekezwa kumwongeza mwakilishi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania kuwa miongoni mwa Wajumbe wa Bodi. Lengo la marekebisho haya ni kupata utaalam kuhusu silaha za kemikali katika bodi, kufuatia kupendekezwa kwa jukumu la usimamizi wa silaha za kikemikali kutekelezwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 11 kinarekebishwa kwa lengo la kupanua wigo wa utunzaji wa taarifa za kikemikali na wauzaji wa kemikali katika rejesta. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182 ambapo wigo wa usimamizi wa kemikali kwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali umeongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ya muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182. Kifungu cha pili kinapendekezwa kurekebishwa katika tafsiri ya neno "*chemical*" ili kujumuisha silaha za kikemikali na viuatilifu dhurifu vya afya ya jamii. Vilevile inapendekezwa kuongeza misamiati mipya iliyotumika katika Sheria hii. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi na tafsiri sahihi za misamiati iliyotumika katika sheria kufuatia marekebisho yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa ili kujumuisha matakwa ya Mfumo wa Ulinganifu wa Kimataifa wa Uainishaji na Uwekaji Lebo wa Kemikali *(GHS)* na orodha ya viuatilifu dhurifu vya afya ya jamii. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti yanayohusiana na viwango vya kimataifa vya uainishaji na uwekaji lebo wa kikemikali ili kuimarisha utekelezaji wa sheria katika kulinda afya na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 12 kinapendekezwa kufutwa ili kuondoa mwingiliano wa vifungu vya 11 na 12. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha vifungu hivyo ili kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya majaribio ya uwandani ya viuatilifu dhurifu vya afya ya jamii. Lengo la marekebisho haya ni kupima ubora na usalama wa viuatilifu dhurifu vya afya ya jamii kabla havijasajiliwa. Aidha, kifungu kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha msajili kutumia taarifa za tathmini kutoka nchi nyingine zenye mfumo wa udhibiti unaofanana na Tanzania wakati wa usajili. Lengo la marekebisho haya ni

kurahisisha mchakato wa usajili wa kemikali ambazo zimesajiliwa nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 52(a) kinapendekezwa kuongezwa ili kumwezesha Msajili kuweka zuio la muda kwa viuatilifu vya afya ya jamii ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu na mazingira yetu. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ubora na usalama wa viuatilifu vya afya ya jamii vinavyotumika hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jedwali la Kwanza linapendekezwa kurekebishwa kwa kumwongeza mwakilishi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania mwenye ujuzi wa masuala ya silaha za kikemikali kama Mjumbe wa Bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha ufanisi wa bodi katika utekelezaji majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano ya muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413, ambapo kifungu cha tano kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta majukumu yanayohusiana na uratibu wa shughuli za usalama wa usafiri wa ardhini na uthibitishaji wa ubora wa magari ya huduma za umma na kuipa mamlaka wajibu wa kuthibitisha ubora wa miundombinu ya reli. Lengo la marekebisho haya ni kuepuka mwingiliano wa majukumu ya udhibiti kati ya mamlaka na Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka tafsiri sahihi ya msamiati "*conflict of interest*" kwa kubainisha masuala ambayo yanapelekea kuwepo kwa mgongano wa maslahi. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kukiwianisha na masharti ya kifungu cha 27 kinachoruhusu mamlaka kufanya mapitio ya maamuzi yake. Lengo la marekebisho haya ni kupanua wigo wa jopo linalohusika na mapitio ili kulipa uwezo wa kupitia maamuzi yaliyofanywa na Mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 29 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupunguza idadi ya Wajumbe wa Baraza kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji wa Baraza. Aidha, kifungu kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumpa Waziri mamlaka ya kumteua mwenyekiti. Lengo la marekebisho haya ni kumwongezea ulinzi mwenyekiti katika kutekeleza na kusimamia majukumu ya Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 30 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha muda wa kuhudumu kama Wajumbe katika Baraza. Lengo la marekebisho haya ni kutunza na kuhifadhi kumbukumbu za kiutendaji za shughuli za Baraza. Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha Sekretarieti ya Baraza kuundwa kutoka miongoni mwa watumishi wa Baraza. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya sita ya muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Sura ya 150 ambapo kifungu cha saba kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa mamlaka ya bodi ya kuteua na kuamua ajira za Wakuu wa Idara na kuwianisha masharti ya Kifungu hiki na kifungu cha 12 kuhusiana na mamlaka ya nidhamu. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha na kuwianisha masharti na muundo wa utawala wa hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha nane kinapendekezwa kurekebishwa ili kutambua mamlaka ya Rais katika uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji. Lengo la marekebisho haya ni kukuza utawala bora na uwajibikaji katika usimamizi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya 11 na 15 vinapendekezwa kurekebishwa ili kutambua "vitengo" kama sehemu ya muundo wa utawala wa hospitali na kuboresha masharti kuhusiana na Kamati ya Usimamizi wa Hospitali. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika usimamizi wa hospitali hii muhimu kwa Taifa letu. Aidha, kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuanzisha Kamati ya Utawala ya Hospitali. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha

ubora wa huduma za afya, ufanisi wa kiutendaji na uwajibikaji ndani ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwianisha mamlaka ya nidhamu ya Mkurugenzi Mtendaji na Bodi kwa wafanyakazi wote wa hospitali hii muhimu. Lengo la marekebisho haya ni kuepuka kuingiliana kwa mamlaka ya nidhamu juu ya wafanyakazi wa hospitali na kuongeza uwajibikaji bora na ufanisi kwa wafanyakazi wa hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 16 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuondoa sharti la lazima kwa bodi kuwekeza katika uwekezaji unaoruhusiwa katika Sheria ya Uwekezaji wa Wadhamini. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa uwekezaji wa hospitali na kuiwezesha kujiendesha kibiashara kama taasisi ya kimkakati kwa kuzingatia maelekezo yatakayokuwa yanatolewa na Msajili wa Hazina na mamlaka nyingine zozote zinazohusika. Vilevile jedwali linapendekezwa kurekebishwa katika muundo wa bodi na mamlaka ya uteuzi wa wajumbe wa bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na miongozo ya Msajili wa Hazina kuhusu uendeshaji wa mashirika ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya saba ya muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Sura ya 59 ambapo kifungu cha pili kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri mpya ya msamiati "*medical research*" kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa tafsiri iliyokusudiwa katika masharti mbalimbali ya Sheria. Kifungu cha nne kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza mawanda ya utafiti na matokeo ya utafiti kwa kujumuisha tafiti nyingine za afya zinazokusudia kuzuia magonjwa, kuimarisha ubora wa huduma za afya na kuimarisha huduma na mifumo ya afya. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza vipengele muhimu katika hatua za kudhibiti magonjwa ili kutatua changamoto za kiafya za Watanzania kwa ufanisi kupitia tafiti za kina na hatimaye kuboresha afya na ustawi wa wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha tano kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo wa masharti ya sheria kwa

kuwezesha kufanyika kwa tafiti za magonjwa ya binadamu kwenye vituo vingine visivyo vya utafiti wa magonjwa ya binadamu kama vinavyoweza kutangazwa na Waziri kuwa ni vituo vya utafiti. Lengo la marekebisho haya ni kuhamasisha ubunifu na maendeleo kwa kuunganisha mitazamo tofauti, mbinu mbalimbali na rasilimali katika tafiti zinazohusu magonjwa ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya nane na 16 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuendana na muundo mpya wa taasisi uliopitishwa ambao ulibadilisha cheo cha Mkurugenzi wa Kituo kuwa Meneja wa Kituo. Vilevile kifungu kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa mamlaka ya meneja wa vituo ya kuajiri. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na muundo mpya wa taasisi uliopitishwa, ambapo meneja wa vituo hawana mamlaka ya kuajiri watumishi wa kada saidizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya 10 na 12 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha masharti ya adhabu. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha adhabu zinatolewa kwa kuzingatia thamani ya sasa ya fedha na ukubwa wa kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha utaratibu wa kutoa motisha kwa wafanyakazi wa taasisi wanaofanya uvumbuzi na kuzalisha bidhaa kutokana na tafiti zilizofanywa na taasisi. Lengo la marekebisho haya ni kuhamasisha uendelezaji wa matokeo ya utafiti ili kupata bidhaa kamili kwa manufaa ya umma kwa ujumla na mtafiti mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 17 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuruhusu Wajumbe wa Baraza la Taasisi ambao ni watumishi wa umma kulipwa posho na stahili nyingine sawa na wajumbe wengine wakati wakitekeleza majukumu ya baraza. Lengo la marekebisho haya ni kuweka usawa wa malipo kwa Wajumbe wa Baraza hivyo kuongeza ufanisi wa baraza katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nane ya muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268, ambapo vifungu vya 3, 7(b) na 8(b) vya Sheria vinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta cheo na majukumu ya Naibu Mwandishi Mkuu wa Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na muundo ulioidhinishwa wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kupitia Jedwali la Marekebisho la Serikali, inapendekezwa kurekebisha kifungu cha nane cha sheria hiyo ili kuongeza majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusiana na ushauri na usimamizi wa mikataba. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha na kuleta tija katika utekelezaji wa mikataba inayoingiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tisa ya muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Bandari, Sura ya 166, ambapo sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla kwa kubadilisha maneno *"security officer"* na kuwa *"port security officer."* Lengo la marekebisho haya ni kuzingatia Kanuni za Kimataifa za Usalama wa Meli na Vituo vya Bandari za mwaka 2004 *(ISPS Code)* zilizotengenezwa kutokana na Mkataba wa Kimataifa wa Usalama wa Maisha Baharini wa Mwaka 1974 *(SOLAS Convention)* ambao Tanzania ni mwanachama wa mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha tatu kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kufuta tafsiri ya neno *seamen*. Marekebisho haya yanalenga kufuta tafsiri ya neno ambalo halijatumika katika sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza majukumu ya bandari kuhusiana na kusimamia taasisi ya mafunzo kwa ajili ya kuendeleza tafiti na kujenga uwezo katika sekta ya baharini na bandari. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha usimamizi bora na wa ufanisi wa bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 38A kinapendekezwa kurekebishwa ili kutoa mamlaka kwa Mamlaka ya Bandari

kutengeneza kanuni kuhusiana na usimamizi na uendeshaji wa taasisi ya mafunzo. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha usimamizi na ufanisi wa taasisi ya mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 44 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuongeza mawanda ya mamlaka ya Waziri ya kutengeneza kanuni. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 60A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti ya kuundwa kwa Kamati ya Usalama wa Bandari, ambayo itakuwa na jukumu la kuratibu mawasiliano ya bandari, utambuzi wa hatari na uratibu wa rasilimali za kupunguza vitisho na matukio ya majanga yanayohusiana na bandari. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha uwepo wa usimamizi bora wa bandari na uzingatiaji wa Kanuni za Kimataifa za Usalama wa Meli na Vituo vya Bandari ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 86A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka adhabu ya jumla kwa makosa ambayo hayajawekewa adhabu mahususi katika sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 89 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya kwa kuainisha hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa dhidi ya baharia, mmiliki wa chombo cha usafiri baharini au kiongozi wa chombo kutokana na kusababisha madhara katika miundombinu ya bandari. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha usalama wa miundombinu ya bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 10 ya muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Utoaji wa Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317. Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla kwa kubadilisha misamiati "*uneconomic competition*" popote yalipotumika katika sheria na kuweka maneno "*unfair competition*." Lengo la marekebisho haya ni kuweka msamiati

sahihi unaoendana na mifumo ya soko huria ya ndani na ya kimataifa inayotambua ushindani wa haki na usio wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha tatu kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta tafsiri za misamiati "*Appointing Authority, Central Licencing Authority, Member, Regional Licencing Authority* na *Urban Area,*" kufuatia kufutwa kwa masharti ndani ya sheria yaliyokuwa yametumia misamiati hiyo. Aidha, kifungu kinarekebishwa kwa kuongeza misamiati mipya iliyotumika katika masharti mbalimbali ya sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha misamiati inayotumika katika sheria inaeleweka kwa urahisi na inaendana na masharti ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya nne na tano vinapendekezwa kurekebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya ili kutambua Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini kama Mamlaka yenye dhamana ya kutoa, kuhuisha, kusitisha, kufuta leseni na kuwaruhusu mawakala waidhiniwa kutoa huduma za utoaji na uhuishaji wa leseni au vibali. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi na upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya 5A, 6, 6A, 7, 8, 9, 10, 18, 19, 20 na 21 vinapendekezewa kufutwa kwa sababu Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini imepewa majukumu ya kutoa, kuhuisha na kufuta leseni au vibali chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413. Vilevile utaratibu wa uombaji wa leseni umeainishwa kwenye sheria hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kutatua changamoto ya mwingiliano wa majukumu ya utoaji leseni na udhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa masharti ya adhabu zinazohusu leseni maalum kwa kuwa adhabu hizo zimeainishwa kwenye Kanuni za Leseni za Usafiri wa Umma za mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 28 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza adhabu. Lengo la marekebisho haya ni kulinganisha adhabu hiyo na thamani ya sasa ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 34 kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa masharti yake yamepitwa na wakati na kwa kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini ndiyo yenye mamlaka ya kufuta na kusitisha leseni na siyo Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya 36, 37, 38, 39 na 40 vinapendekezwa kufutwa kwa kuwa utaratibu wa utoaji leseni, uwasilishaji wa pingamizi la maombi au mabadiliko ya leseni hayashughulikiwi chini ya Sheria hii na utaratibu wa kushughulikia malalamiko na rufaa umeainishwa kwenye Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti ya Sheria hii na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 41 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuondoa makosa ambayo yapo kwenye kanuni za adhabu, Sura ya 16 na kuweka masharti ya adhabu ya jumla kwa makosa ambayo adhabu mahususi haijatolewa kwenye sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya 42, 43 na 44 vinapendekezwa kufutwa kwa sababu makosa hayo yana adhabu ya jumla na kosa la kutoza nauli zaidi adhabu yake imeainishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini pamoja na kanuni zake. Vilevile masuala ya fedha na ada yameainishwa katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa takwa la ushiriki wa washauri wa baraza kufuatia mabadiliko ya mamlaka ya utoaji wa leseni. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 46 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuondoa mamlaka ya Maafisa Tawala kushiriki katika ukaguzi wa vyombo vya usafiri. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa utekelezaji wa majukumu

chini ya kifungu hicho yanatekelezwa na polisi na maafisa wa mamlaka pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya 48 na 49 vinapendekezwa kufutwa kufuatia mapendekezo ya marekebisho ya kufutwa kwa vifungu vya 36, 37, 38, 39 na 40. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na mapendekezo ya marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413 ambapo masuala yanayohusiana na leseni, na utatuzi wa migogoro yanasimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hotuba hii na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments Bill, 2025)* na kuupitisha pamoja na marekebisho yake katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na mara ya tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA HAMZA S. JOHARI (MB), MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI WA MWAKA 2025 (THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) BILL, 2025) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote, naomba kabla ya kutoa hotuba kuhusu Muswada huu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema; na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge, na kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025).

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya**

**Muungano wa Tanzania** kwa kuendelea kuiongoza Nchi kwa umahiri, mafanikio makubwa na uzalendo wa hali ya juu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, kumpongeza Mhe. Naibu Spika na kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Ninapenda kuungana na Watanzania wenzangu pia kumpongeza Prof. Mohamed Yakub Janabi kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika katika Shirika la Afya Duniani na kupeperusha vema bendera ya Tanzania katika tasnia ya afya ulimwenguni. Ninamtakia heri katika majukumu yake mapya.

**Mheshimiwa Spika**, Kipekee niishukuru sana Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti, **Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama** (Mb.) na Makamu wake **Mhe. Florent Laurent Kyombo (Mb.)** pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa umakini na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati

na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Afya na Wizara ya Uchukuzi na wadau wengine wote kwa ushirikiano waliotupatia katika mchakato mzima wa kushughulikia Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025)* ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Tisa (9) zifuatazo:

(a) Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa

(b) Kupangwa, Sura ya 200;

(c) Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa

(d) Serikali, Sura ya 177;

(e) Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182;

(f) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413;

(g) Sheria ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Sura ya 150;

(h) Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Sura ya 59;

(i) Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya

(j) Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268;

(k) Sheria ya Bandari, Sura ya 166; na

(l) Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo Sheria zinapendekezwa kurekebishwa katika Sehemu zake.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200, ambapo kifungu cha 26 kinapendekezwa kufutwa. Marekebisho haya yanakusudia kuwezesha mashtaka chini ya Sheria hii kufunguliwa bila kuhitaji ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Takwa la ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka kabla ya kufungua shtaka chini ya Sheria hii liliwekwa miaka ya nyuma ambapo sehemu kubwa ya mashtaka yalikuwa yanaendeshwa na askari polisi kwa kuwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka haikuwa imeenea katika mikoa na wilaya zote nchini. Hivyo, kulikuwa na umuhimu wa kupata ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka ili kudhibiti ufunguaji holela wa mashtaka. Katika mazingira ya sasa ambapo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imefungua ofisi zake hadi ngazi ya Wilaya na kesi zote za jinai zinaendeshwa na Mawakili wa Serikali wanaowajibika moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, masharti ya kupata ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka yanakosa mantiki ya kuendelea kuwepo na yanaweza kuchangia ucheleweshaji wa haki jinai.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sura ya 177. Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutafsiri upya msamiati "chemical" kwa kuwianisha tafsiri ya msamiati huo na tafsiri ya msamiati "chemical" iliyotolewa katika Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182. Lengo la marekebisho haya ni kutoa tafsiri itakayojumuisha masuala ya silaha za kikemikali yanayopendekezwa kuongezwa katika wigo wa Sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 7 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kupunguza mwakilishi mmoja kutoka taasisi za elimu ya juu au taasisi za utafiti kama mjumbe wa Bodi na kubaki na mwakilishi mmoja kutoka katika taasisi hizo kwa kuwa taasisi hizo tayari zina uwakilishi katika Kamati za Kitaalam ikiwemo Kamati ya Kitaalamu

ya Usimamizi wa Kemikali, Kamati ya Kitaalamu ya Udhibiti wa Vinasaba vya Binadamu na Kamati ya Kitaalamu ya Kudhibiti Matukio ya Sumu ambazo kazi zake ni kuishauri Bodi. Vilevile, inapendekezwa kumwongeza mwakilishi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania kuwa miongoni mwa wajumbe wa Bodi. Lengo la marekebisho haya ni kupata utaalamu kuhusu silaha za kemikali katika Bodi kufuatia kupendekezwa kwa jukumu la usimamizi wa silaha za kemikali kutekelezwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 11 kinarekebishwa kwa lengo la kupanua wigo wa utunzaji wa taarifa za kemikali na wauzaji wa kemikali katika rejesta. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182, ambapo wigo wa usimamizi wa kemikali kwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali umeongezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182. Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa katika tafsiri ya neno “chemical” ili kujumuisha silaha za kikemikali na viuatilifu dhurifu vya afya ya jamii. Vilevile, inapendekezwa kuongeza misamiati mipya iliyotumika katika Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi na tafsiri sahihi za misamiati iliyotumika katika Sheria kufuatia marekebisho yanayopendekezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa ili kujumuisha matakwa ya Mfumo wa Ulinganifu wa Kimataifa wa Uainishaji na Uwekaji Lebo wa Kemikali (GHS) na orodha ya viuatilifu dhurifu vya afya ya jamii. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti yanayohusiana na viwango vya kimataifa vya uainishaji na uwekaji lebo wa kemikali ili kuimarisha utekelezaji wa Sheria katika kulinda afya na mazingira. Kifungu cha 12 kinapendekezwa kufutwa ili kuondoa mwingiliano wa vifungu vya 11 na 12. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha vifungu hivyo ili kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya majaribio ya uwandani ya viuatilifu dhurifu vya afya ya jamii. Lengo la marekebisho haya ni kupima ubora na usalama wa viuatilifu dhurifu vya afya ya jamii kabla havijasajiliwa. Aidha, kifungu kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha Msajili kutumia taarifa za tathmini kutoka nchi nyingine zenye mfumo wa udhibiti unaofanana na Tanzania wakati wa usajili. Lengo la marekebisho haya ni kurahisisha mchakato wa usajili wa kemikali ambazo zimesajiliwa nje ya Tanzania.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kifungu cha 52A kinapendekezwa kuongezwa ili kumwezesha Msajili kuweka zuio la muda kwa viuatilifu vya afya ya jamii ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu na mazingira. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ubora na usalama wa viuatilifu vya afya ya jamii vinavyotumika nchini. Jedwali la Kwanza linapendekezwa kurekebishwa kwa kumwongeza mwakilishi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania mwenye ujuzi wa masuala ya silaha za kikemikali kama mjumbe wa Bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha ufanisi wa Bodi katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413, ambapo kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta majukumu yanayohusiana na uratibu wa shughuli za usalama wa usafiri wa ardhini na uthibitishaji wa ubora wa magari ya huduma za umma na kuipa Mamlaka wajibu wa kuthibitisha ubora wa miundombinu ya reli. Lengo la marekebisho haya ni kuepuka mwingiliano wa majukumu ya udhibiti kati ya Mamlaka na Wizara ya Mambo ya Ndani. Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka tafsiri sahihi ya msamiati "conflict of interest" kwa kubainisha masuala ambayo yanapelekea kuwepo kwa mgongano wa maslahi. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Bodi.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kukiwianisha na masharti ya kifungu cha 27 kinachoruhusu Mamlaka kufanya mapitio ya maamuzi yake. Lengo la marekebisho haya ni kupanua wigo wa jopo

linalohusika na mapitio ili kulipa uwezo wa kupitia maamuzi yaliyofanywa na Mamlaka. Kifungu cha 29 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupunguza idadi ya wajumbe wa Baraza kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji wa Baraza. Aidha, kifungu kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumpa Waziri mamlaka ya kumteua Mwenyekiti. Lengo la marekebisho haya ni kumwongezea ulinzi Mwenyekiti katika kutekeleza na kusimama maamuzi ya Baraza.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 30 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha muda wa kuhudumu wa wajumbe katika Baraza. Lengo la marekebisho haya ni kutunza na kuhifadhi kumbukumbu za kiutendaji za shughuli za Baraza. Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha Sekretarieti ya Baraza kuundwa kutoka miongoni mwa watumishi wa Baraza. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Baraza.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Sura ya 150, ambapo kifungu cha 7 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa mamlaka ya Bodi ya kuteua na kuamua ajira za wakuu wa idara na kuwianisha masharti ya kifungu hiki na kifungu cha 12 kuhusiana na mamlaka ya nidhamu. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha na kuwianisha masharti na muundo wa utawala wa Hospitali. Kifungu cha 8 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutambua mamlaka ya Rais katika uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji. Lengo la marekebisho haya ni kukuza utawala bora na uwajibikaji katika usimamizi wa Hospitali.

**Mheshimiwa Spika**, Vifungu vya 11 na 15 vinapendekezwa kurekebishwa ili kutambua "vitengo" kama sehemu ya muundo wa utawala wa Hospitali na kuboresha masharti kuhusiana na Kamati ya Usimamizi wa Hospitali. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika usimamizi wa Hospitali. Aidha, kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuanzisha Kamati ya Utawala ya Hospitali. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ubora wa huduma za afya, ufanisi wa kiutendaji na uwajibikaji ndani ya Hospitali.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwianisha mamlaka ya nidhamu ya Mkurugenzi Mtendaji na Bodi kwa wafanyakazi wote wa Hospitali. Lengo la marekebisho haya ni kuepuka kuingiliana kwa mamlaka ya nidhamu juu ya wafanyakazi wa Hospitali na kuongeza uwajibikaji bora na ufanisi kwa wafanyakazi.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 16 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuondoa sharti la lazima kwa Bodi kuwekeza katika uwekezaji unaoruhusiwa katika Sheria ya Uwekezaji wa Wadhamini. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa uwekezaji wa Hospitali na kuiwezesha kujiendesha kibiashara kama taasisi ya kimkakati kwa kuzingatia maelekezo yatakayokuwa yanatolewa na Msajili wa Hazina na mamlaka nyingine zozote zinazohusika. Vilevile, Jedwali linapendekezwa kurekebishwa katika muundo wa Bodi na mamlaka ya uteuzi wa wajumbe wa Bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na miongozo ya Msajili wa Hazina kuhusu uendeshaji wa Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Sura ya 59**,** ambapo kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri mpya ya msamiati "medical research" kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa tafsiri iliyokusudiwa katika masharti mbalimbali ya Sheria. Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza mawanda ya utafiti na matokeo ya utafiti kwa kujumuisha tafiti nyingine za afya zinazokusudia kuzuia magonjwa, kuimarisha ubora wa huduma za afya na kuimarisha huduma na mifumo ya afya. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza vipengele muhimu katika hatua za kudhibiti magonjwa ili kutatua changamoto za kiafya za watanzania kwa ufanisi kupitia tafiti za kina na hatimaye kuboresha afya na ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo wa masharti ya Sheria kwa kuwezesha kufanyika kwa tafiti za magonjwa ya binadamu kwenye vituo vingine visivyo vya utafiti wa magonjwa ya binadamu kama vinavyoweza kutangazwa na Waziri kuwa vituo vya utafiti. Lengo la

marekebisho haya ni kuhamasisha ubunifu na maendeleo kwa kuunganisha mitazamo tofauti, mbinu mbalimbali na rasilimali katika tafiti zinazohusu magonjwa ya binadamu.

**Mheshimiwa Spika**, Vifungu vya 8 na 16 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuendana na Muundo mpya wa Taasisi uliopitishwa ambao ulibadilisha cheo cha Mkurugenzi wa Kituo kuwa Meneja wa kituo. Vilevile, kifungu kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa mamlaka ya meneja wa vituo ya kuajiri. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na muundo mpya wa Taasisi uliopitishwa, ambapo meneja wa vituo hawana mamlaka ya kuajiri watumishi wa kada saidizi. Vifungu vya 10 na 12 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha masharti ya adhabu. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha adhabu zinatolewa kwa kuzingatia thamani ya sasa ya fedha na ukubwa wa kosa.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha utaratibu wa kutoa motisha kwa wafanyakazi wa Taasisi wanaofanya uvumbuzi na kuzalisha bidhaa kutokana na tafiti zilizofanywa na Taasisi. Lengo la marekebisho haya ni kuhamasisha uendelezaji wa matokeo ya utafiti ili kupata bidhaa kamili kwa manufaa ya umma kwa ujumla na mtafiti mwenyewe. Kifungu cha 17 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuruhusu wajumbe wa Baraza la Taasisi ambao ni watumishi wa umma kulipwa posho na stahili nyingine sawa na wajumbe wengine wakati wakitekeleza majukumu ya Baraza. Lengo la marekebisho haya ni kuweka usawa wa malipo kwa wajumbe wa Baraza hivyo kuongeza ufanisi wa Baraza katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268, ambapo vifungu vya 3, 7B, na 8B vya Sheria vinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta cheo na majukumu ya Naibu Mwandishi Mkuu wa Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na muundo ulioidhinishwa wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. Vilevile, kupitia Jedwali la Marekebisho la Serikali inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 8 cha Sheria hiyo ili kuongeza majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria

Mkuu wa Serikali kuhusiana na ushauri na usimamizi wa mikataba. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha na kuleta tija katika utekelezaji wa mikataba inayoingiwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Bandari, Sura ya 166, ambapo Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla kwa kubadilisha maneno "security officer" kuwa "port security officer". Lengo la marekebisho haya ni kuzingatia Kanuni za Kimataifa za Usalama wa Meli na Vituo vya Bandari za Mwaka 2004 (ISPS Code) zilizotengenezwa kutokana na Mkataba wa Kimataifa wa Usalama wa Maisha Baharini wa Mwaka 1974, ambao Tanzania ni mwanachama. Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kufuta tafsiri ya neno "seamen". Marekebisho haya yanalenga kufuta tafsiri ya neno ambalo halijatumika katika Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza majukumu ya Mamlaka ya Bandari kuhusiana na kusimamia taasisi ya mafunzo kwa ajili ya kuendeleza tafiti na kujenga uwezo katika sekta ya baharini na bandari. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha usimamizi bora na wa ufanisi wa bandari. Kifungu cha 38A kinapendekezwa kurekebishwa ili kutoa mamlaka kwa Mamlaka ya Bandari kutengeneza kanuni kuhusiana na usimamizi na uendeshaji wa taasisi ya mafunzo. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha usimamizi na ufanisi wa taasisi ya mafunzo.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 44 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuongeza mawanda ya mamlaka ya Waziri ya kutengeneza Kanuni. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria. Kifungu cha 60A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti ya kuundwa kwa Kamati ya Usalama wa Bandari, ambayo itakuwa na jukumu la kuratibu mawasiliano ya bandari, utambuzi wa hatari na uratibu wa rasilimali za kupunguza vitisho na matukio ya majanga yanayohusiana na bandari. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha uwepo wa usimamizi bora wa bandari na uzingatiaji wa Kanuni za Kimataifa za Usalama wa Meli na Vituo vya Bandari ya mwaka 2004.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu kipya cha 86A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka adhabu ya jumla kwa makosa ambayo hayajawekewa adhabu mahsusi katika Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria. Aidha, kifungu cha 89 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya kwa kuainisha hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa dhidi ya baharia, mmiliki wa chombo cha usafiri baharini au kiongozi wa chombo kutokana na kusababisha madhara katika miundombinu ya bandari. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha usalama wa miundombinu ya bandari.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Utoaji wa Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317. Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla kwa kubadilisha misamiatia "uneconomic competition" popote yalipotumika katika Sheria na kuweka maneno "unfair competition". Lengo la marekebisho haya ni kuweka msamiati sahihi unaoendana na mifumo ya soko huria ya ndani na ya kimataifa inayotambua ushindani wa haki na usio wa haki.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 3 kinapendezwa kurekebishwa kwa kufuta tafsiri za misamiati "appointing authority", "Central Licencing Authority", "member", "Regional Licencing Authority" na "urban area", kufuatia kufutwa kwa masharti ndani ya Sheria yaliyokuwa yametumia misamiati hiyo. Aidha kifungu kinarekebishwa kwa kuongeza misamiati mipya iliyotumika katika masharti mbalimbali ya Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha misamiati inayotumika katika Sheria inaeleweka kwa urahisi na inaendana na masharti ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413.

**Mheshimiwa Spika**, Vifungu vya 4 na 5 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya ili kutambua Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini kama Mamlaka yenye dhamana ya kutoa, kuhuisha, kusitisha na kufuta leseni na kuwaruhusu mawakala waidhiniwa kutoa huduma za utoaji na uhuishaji wa leseni au vibali. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi na upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Vifungu vya 5A, 6, 6A, 7, 8, 9, 10, 18, 19, 20 na 21 vinapendekezewa kufutwa kwa sababu Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini imepewa majukumu ya kutoa, kuhuisha na kufuta Leseni au vibali chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413. Vilevile, utaratibu wa uombaji wa leseni umeainishwa kwenye Sheria hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kutatua changamoto ya mwingiliano wa majukumu ya utoaji leseni na udhibiti. Kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa masharti ya adhabu zinazohusu leseni maalumu kwa kuwa adhabu hizo zimeainishwa kwenye Kanuni za Leseni za Usafiri wa Umma za Mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 28 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza adhabu. Lengo la marekebisho haya ni kulinganisha adhabu hiyo na thamani ya sasa ya fedha. Kifungu cha 34 kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa masharti yake yamepitwa na wakati na kwa kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini ndiyo yenye mamlaka ya kufuta na kusitisha leseni na siyo Waziri.

**Mheshimiwa Spika**, Vifungu vya 36, 37, 38, 39 na 40 vinapendekezwa kufutwa kwa kuwa utaratibu wa utoaji leseni, uwasilishaji wa pingamizi la maombi au mabadiliko ya leseni hayashughulikiwi chini ya Sheria hii na utaratibu wa kushughulikia malalamiko na rufaa umeainishwa kwenye Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti ya Sheria hii na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 41 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuondoa makosa ambayo yapo kwenye Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 na kuweka masharti ya adhabu ya jumla kwa makosa ambayo adhabu mahsusi haijatolewa kwenye Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria. Vifungu vya 42, 43 na 44 vinapendekezwa kufutwa kwa sababu makosa hayo yana adhabu ya jumla na kosa la kutoza nauli zaidi adhabu yake imeainishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini na kanuni zake. Vilevile, masuala ya fedha na ada yameainishwa katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa takwa la ushiriki wa washauri wa Baraza kufuatia mabadiliko ya mamlaka ya utoaji wa leseni. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria. Kifungu cha 46 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuondoa mamlaka ya maafisa tawala kushiriki katika ukaguzi wa vyombo vya usafiri. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa utekelezaji wa majukumu chini ya kifungu hicho yanatekelezwa na polisi na maafisa wa Mamlaka pekee.

**Mheshimiwa Spika**, Vifungu vya 48 na 49 vinapendekezwa kufutwa kufuatia mapendekezo ya marekebisho ya kufutwa kwa vifungu vya 36, 37, 38, 39 na 40. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na mapendekezo ya marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413 ambapo masuala yanayohusiana na leseni, na utatuzi wa migogoro yanasimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hotuba hii na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments Bill, 2025) na kuupitisha pamoja na marekebisho yake katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Hamza S. Johari (Mb.),
**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**
5 Juni, 2025

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono ahsante Mheshimiwa *AG*. Sasa ninamwita Mwenyekiti.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa

Naibu Spika, awali ya yote ninaomba taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments Bill, 2025)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza ni utangulizi. maelezo ya jumla; kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza Kikao cha Kumi na Nne cha Mkutano wa Kumi na Nane, tarehe 14 Februari, 2025 kwa utaratibu ulioainishwa katika Kanuni ya 96(1). Baada ya hatua hiyo, na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14), ulitumia mamlaka yako kuuleta muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna Kamati ilivyotekeleza jukumu la uchambuzi; uchambuzi wa miswada ya sheria ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilianza uchambuzi kwa kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari, Mbunge, siku ya Jumanne tarehe 4 Machi, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutimiza masharti ya Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati iliwaalika wadau kuwasilisha maoni *(public hearing)* kuhusu muswada huu kwa njia ya kielektroniki au kufika kwenye kikao cha Kamati kilichofanyika siku ya Jumatano tarehe 5 Machi, 2025. Kwa upekee Kamati

inapenda kuwashukuru wadau wote kwa kutoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya muswada kwa kuzingatia maelezo ya mtoa hoja na maoni ya wadau. Aidha, siku ya Jumamosi tarehe 8 Machi, 2025, Kamati ilikutana na Serikali ili kufanya majumuisho kuhusu Ibara mbalimbali za muswada huu kwa kumhusisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria, na watendaji mbalimbali wa taasisi za Serikali zinazohusika na sheria zinazopendekezwa kurekebishwa. Baada ya hapo kwa kuzingatia Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, tulikujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili; uchambuzi wa muswada; maelezo ya awali; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025)* umegawanyika katika sehemu kuu 10 na unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria tisa kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza inahusu masharti ya utangulizi wakati sehemu ya pili hadi sehemu ya 10 zinaweka masharti mbalimbali kwa lengo la kufanya marekebisho yanayopendekezwa katika sheria kuu tisa ambazo zimeainishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilichambua mapendekezo hayo yanayopendekezwa kwa kufanya uchambuzi na upembuzi yakinifu kuhusu marekebisho yanayopendekezwa. Baada ya uchambuzi huo pamoja na majumuisho yaliyofanyika baina ya Kamati na Serikali, Kamati hii kama ilivyokuwa kwa wadau mbalimbali, inakubaliana kwa sehemu kubwa na mapendekezo ya muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilichambua muswada ibara kwa ibara kama zinavyoonekana kwenye muswada na wasilisho la mtoa hoja na kukubaliana na marekebisho hayo isipokuwa kwa ibara chache ambazo Kamati ilihitaji ufafanuzi na majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza ya muswada inahusu masharti ya utangulizi, inayojumuisha ibara ya kwanza inayohusu jina fupi na ibara ya pili inayoelezea marekebisho yanayopendekezwa kufanyika katika sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilichambua ibara zote na kubaini ibara chache zenye hoja za msingi ambazo zilihitaji ufafanuzi kutoka kwa mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara hizo zimechambuliwa hapa chini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni ibara ya sheria zenye mapungufu zinazofanyiwa marekebisho na maudhui yake; wakati tunafanya uchambuzi wa muswada huu pamoja na maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika sheria nane kati ya sheria tisa zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyowasilishwa na mtoa hoja. Sheria hizo nane ambazo Kamati ilizibaini kuwa na mapungufu zimebainishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200; marekebisho ya sheria hii yanapatikana katika sehemu ya pili ya muswada kuanzia ibara ya tatu hadi ibara ya nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya tatu inaweka sharti kuwa sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200, wakati ibara ya nne ya muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 26 cha sheria hii ili kuondoa sharti kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka kutoa ridhaa kabla ya kufungua mashtaka ya makosa yaliyoainishwa katika Sheria hii. Sheria ilivyo sasa, kifungu cha 26(1)

kimempa mamlaka Mkurugenzi wa Mashtaka kwa nafasi yake kutoa ridhaa hiyo na siyo mtu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182; marekebisho ya sheria hii yanapatikana katika sehemu ya nne ya muswada kuanzia ibara ya tisa hadi ibara ya 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 14 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 52 kwa kuongeza kifungu cha 52A kinachotoa mamlaka kwa Msajili wa Dawa ya kuweka zuio la muda kwa viuatilifu vya afya ya jamii ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu na mazingira. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ubora na usalama wa viuatilifu vya afya ya jamii vinavyotumika nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413; sehemu hii inahusu ibara ya 16 hadi ya 22 ya muswada. Ibara ya 17 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 5 kwa kufuta majukumu yanayohusiana na uratibu wa shughuli za usalama wa usafiri wa ardhini na uthibitishaji wa ubora wa magari ya huduma za umma na kuipa mamlaka wajibu wa kuthibitisha ubora wa miundombinu ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho haya ni kuondoa baadhi ya shughuli za uratibu kwa kuwa zinasimamiwa na sheria nyingine. Kwa mfano, kuondoa adhabu zinazotokana na mwendokasi na uthibitishaji wa vyombo vya moto kutumika barabarani unaosimamiwa na Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168. Pia kuipa nguvu Sheria ya *LATRA* kusimamia sheria ambazo hazikutajwa katika kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura 413.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 21 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 30, ili kubainisha muda wa kuhudumu kwa wajumbe katika baraza ambapo kwa mwenyekiti inapendekezwa kuwa miaka minne na kwa wajumbe miaka mitatu. Lengo la marekebisho ni kutofautisha muda wa kuhudumu

katika baraza, ili kutunza na kuhifadhi kumbukumbu za kiutendaji za shughuli za baraza *(stagger principle)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, Sura ya 150; sehemu hii inahusu ibara ya 23 na ibara ya 30. Ibara ya 23 inaeleza kuwa, sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, Sura ya 150. Aidha, kwa ujumla, sehemu hii inalenga kuboresha Sheria ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, ili kuboresha ufanisi wa hospital kuendana na wakati uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ibara zote zinazofanyia marekebisho sheria hii, kamati ilikuwa na hoja katika ibara ya 29, ambayo inafuta na kuandika upya kifungu cha 16 cha sheria, ili kuondoa sharti la lazima kwa bodi kuwekeza katika uwekezaji unaoruhusiwa katika Sheria ya Uwekezaji wa Wadhamini. Lengo la marekebisho ni kuongeza wigo wa uwekezaji wa hospitali kwa kuzingatia maelekezo yatakayokuwa yanatolewa na Msajili wa Hazina na mamlaka nyingine zozote zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Sura ya 59; ibara ya 32 inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 2 cha sheria, ili kuongeza tafsiri ya msamiati "*medical research*" ambao haukuwepo, ili kuongeza uelewa wa maana iliyokusudiwa katika masharti mbalimbali ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhima kuu ya sheria ni kuanzisha Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu. Sheria inafafanua maana ya taasisi na maneno mengine bila ya kutoa maana ya *medical research* katika tafsiri za maneno.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268; ibara ya 43 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 7(1)(e) kinachohusu kazi za Naibu Mwanasheria Mkuu kwa kuweka neno "*appointment*" kabla ya neno "*discipline*." Lengo la marekebisho haya ni kumuongezea Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali jukumu la kuteua Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Bandari, Sura ya 166; ibara ya 51 inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 44 cha sheria, ili kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni. Sheria ilivyo sasa; kifungu cha 44(1) kinampa mamlaka Waziri kutengeneza kanuni na kifungu cha 44(2) kinaweka sharti la kanuni hizo kutangazwa katika Gazeti la Serikali, ili zipate uhalali wa kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 53 inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 86 kwa kuongeza kifungu kipya cha 86A, ili kuweka adhabu ya jumla kwa makosa ambayo hayajawekewa adhabu mahsusi katika sheria kuwa, isiyopungua shilingi 10,000,000 na isiyozidi shilingi 50,000,000 au kifungo kisichopungua miezi 12 na kisichozidi miaka miwili au vyote. Aidha, sheria ilivyo sasa katika kifungu cha 86 cha sheria hii, haihitaji kiwango cha adhabu anachopewa mtu aliyetenda kosa lililoainishwa katika kifungu hicho, ombwe hili pia, linaonekana katika kifungu cha 66 cha sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Utoaji wa Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317; ibara ya 59 inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu cha 5, ili kuruhusu mawakala waidhiniwa kutoa huduma za utoaji na uhuishaji wa leseni au vibali mtawalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ilivyo sasa katika kifungu cha 5 kinahamisha mamlaka yote aliyopewa Waziri kisheria, ili yasimamiwe na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini. Ibara ya 67 inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu cha 46, ili kuipa Mamlaka ya Leseni uwezo wa kukagua magari, ambapo afisa wa polisi au afisa wa mamlaka, kwa madhumuni ya kuhakikisha utekelezaji wa sheria hii atakuwa na uwezo wa:-

(i) kukagua gari lolote;

(ii) kudai kuoneshwa nyaraka au rekodi yoyote inayotakiwa kubebwa ndani ya gari hilo; na

(iii) kumtaka dereva au mtu yeyote aliyepo ndani ya gari kutoa taarifa yoyote anayoihitaji afisa wa polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kuhakikisha kuwa utekelezaji wa majukumu chini ya kifungu hicho yanatekelezwa na polisi na maafisa wa mamlaka pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu, maoni na ushauri wa Kamati; maoni ya jumla; kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi, ili kuuboresha muswada huu, kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200; kwenye ibara ya 4 ya muswada Kamati iliishauri Serikali kifungu cha sheria kibakie kama kilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mashauri yote yanayohitaji ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchi nzima ni lazima yafike kwa Mkurugenzi wa Mashtaka mwenyewe, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho yanayoondoa sharti hilo kwa kuwa yataondoa mlundikano wa mahabusu gerezani. Ni maoni ya Kamati kwamba marekebidho haya yamejikita katika misingi ya haki jinai ambayo yanaakisi falsafa za *4R* za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambazo ni maridhiano *(reconciliation),* ustahimilivu *(resiliency),* mabadiliko *(reforms)* na kujenga upya *(rebulding)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa moja ya mkakati mahususi wa falsafa hii ni kuimarisha utawala bora, demokrasia na uchumi nchini kwa kupitia upya sera na sheria kwa maendeleo mapana ya Taifa letu, Kamati inakubaliana na marekebisho yanayopendekezwa na mtoa hoja. Aidha, kutokana na majadiliano yaliyofanyika kati ya Kamati na Serikali, Kamati imeridhia maboresho yabaki kama yalivyo, ili kuondoa tatizo la ucheleweshaji wa haki jinai na mlundikano wa mahabusu gerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182; kwenye ibara ya 14 ya muswada, Kamati ilipendekeza kufuta neno "*may*" linaloonekana baada ya neno "*registar*" na badala yake kuweka neno "*shall*", ili kutoa sharti kwa msajili kuzuia matumizi ya viuatilifu baada ya kubaini kuwa, vinaweza kuhatarisha afya na usalama wa jamii, wanyama au mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea ufafanuzi wa Serikali na kutokana na majibu ya Serikali, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho, kama yalivyotolewa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413; katika ibara ya 17, Kamati iliomba kupata ufafanuzi wa sababu zilizosababisha Serikali kuondoa majukumu yanayohusiana na uratibu wa shughuli za usalama wa usafiri wa ardhini na uthibitishaji wa ubora wa magari ya huduma za umma na kuipa mamlaka wajibu wa kuthibitisha ubora wa miundombinu ya reli pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea ufafanuzi wa Serikali. Kutokana na majibu ya Serikali, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho, kama yalivyotolewa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya jumla kuhusu Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413; ni maoni ya Kamati kuwa Serikali itafute suluhu ya mwingiliano uliopo baina ya taasisi mbalimbali za Serikali zinazosimamia sekta ya usafirishaji kwa njia ya barabara kama vile Jeshi la Polisi, *LATRA, TARURA, TANROADS* na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, mkanganyiko ambao umekuwa ukisababisha kadhia kwa wananchi kwa kutozwa faini na mamlaka tofauti kwa kosa moja. Aidha, muingiliano wa kuitendaji kwa taasisi hizi umekuwa ukififisha jitihada za Mheshimiwa Rais za kuchagiza upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali ifanye rejea ya Sheria zote zinazosimamia *LATRA* na Jeshi la Polisi, ili kuiwezesha *LATRA* kusimamia udhibiti wa usafiri ardhini na Jeshi la Polisi kusimamia uratibu wa usalama barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati inaishauri Serikali kuanza matumizi ya mifumo ya kidigitali katika usimamizi wa sheria za usalama barabarani ili kukabiliana na masuala ya rushwa katika usimamizi na utekelezaji wa sheria. Katika ibara ya 21 inayofanya marekebisho katika kifungu cha 30, Kamati iliishauri Serikali marekebisho yanayopendekezwa yaakisi mfumo wa kutunza kumbukumbu za kiutendaji za shughuli za baraza *(stagger principle)* katika sheria. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, Sura ya 150. katika ibara ya 29, ambayo inafuta na kuandika upya kifungu cha 16 cha sheria, ili kuondoa sharti la lazima kwa bodi kuwekeza katika uwekezaji unaoruhusiwa katika Sheria ya Uwekezaji wa Wadhamini, Kamati ilipendekeza kufutwa sharti la Bodi ya Hospitali ya Muhimbili kuzingatia maelekezo yatakayokuwa yanatolewa na Msajili wa Hazina na mamlaka nyingine zote zinazohusika wakati wa uwekezaji. Pia Kamati ilikuwa na maoni kuwa sheria isimpe mamlaka Msajili wa Hazina ya kutoa ridhaa ya bodi kuwekeza, badala yake Msajili wa Hazina apewe taarifa tu. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Sura ya 59; katika ibara ya 32 kamati iliishauri Serikali kuboresha tafsiri ya neno "*medical research*" kwa kufuta maneno "*means measuring the health problem, understating its causes, finding solutions or translating the solutions or scientific evidence into policy*" yanayoonekana mwanzoni mwa tafsiri hiyo na badala yake kuweka maneno "*means the systematic study and investigation conducted to understand, prevent, and address the health problems, with the aim of improving healthcare outcomes,*

*developing treatments and advancing medical knowledge or translating scientific evidence into policy.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya jumla kuhusu Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Sura ya 59; ni maoni ya Kamati kuwa Serikali iongeze jitihada za ufuatiliaji wa tafiti za dawa za asili zitokanazo na miti shamba katika kukabiliana na magojwa mbalimbali yanayoikabili jamii. Aidha, Serikali izithibitishe na kuzitangaza kwa jamii dawa za asili ambazo zitakuwa zimekidhi viwango vya ubora wa matumizi ya matibabu. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268; katika ibara ya 43, Kamati ilipendekeza marekebisho ya kiuandishi kwa kuongeza neno "*and*" baada ya neno "*appoitment*", ili kuleta maana iliyokusudiwa. Hivyo, kifungu hicho kitasomeka "*appoitment and discipline*." Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri wa Kamati na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria Bandari, Sura ya 166; kwenye ibara ya 51 Kamati iliishauri Serikali kufuta aya (f) na (g) za kifungu cha 44(2) kinavyopendekezwa na muswada. Ibara ya 53, Kamati iliishauri Serikali kupunguza adhabu ya chini ya faini kwa makosa ya jumla kutoka shilingi milioni kumi hadi shilingi milioni tatu. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Utoaji wa Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317; kwenye ibara ya 59 Kamati iliomba kupata ufafanuzi kuhusu utaratibu wa upatikanaji na utendaji kazi wa mawakala waidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea ufafanuzi wa Serikali na kutokana na majibu ya Serikali, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho, kama yalivyotolewa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ibara ya 67, Kamati ilipendekeza kumuongeza Afisa wa Mamlaka katika kipengele (c) cha muswada ili kumpa uwezo wa kupata taarifa kutoka kwa dereva au mtu aliye ndani ya chombo cha moto cha umma pale inapohitajika ili kuendana na marekebisho ya sheria yanayopendekezwa. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ambayo ni hitimisho; shukurani; napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wote wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba majina yao yote yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge, kama yalivyooneshwa kwenye taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuliongoza vyema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Mbunge, na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Mbunge, kwa ushirikiano wao mzuri na wa kipekee walioipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inampongeza kwa dhati Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari, Mbunge, akisaidiwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali *(CPD)* Ndugu Onorius Njole kwa kuandaa muswada huu baada ya kubaini makosa mbalimbali katika sheria wakati wa utekelezaji wake. Aidha, Kamati inawashukuru pia kwa ushirikiano walioipatia wakati wa uchambuzi wa muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawashukuru pia watendaji wote chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kutoka taasisi mbalimbali zinazohusika na usimamizi na utekelezaji wa sheria zinazopendekezwa kurekebishwa kwa ushirikiano walioipatia Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa ninawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Ildephonce Leonard, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii na kwa upekee naishukuru sekretarieti ya Kamati iliyohusika na uratibu wa vikao vya uchambuzi wa muswada hadi kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wa Kamati kuhusu hoja; baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025)* pamoja na marekebisho yake, kama ulivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

## MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI WA MWAKA 2025 (*THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) BILL, 2025*) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 99 (5)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Muswada Wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria

Mbalimbali Wa Mwaka 2025 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025*).

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulisomwa Bungeni Mara ya Kwanza kikao cha Kumi na Nne cha Mkutano wa Kumi na Nane, tarehe 14 Februari, 2025 kwa utaratibu ulioainishwa katika **Kanuni ya 96 (1)**. Baada ya hatua hiyo, na kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 97 (1)** ikisomwa pamoja na **Kanuni ya 136 (14)**, ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ili ufanyiwe uchambuzi.

**1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa **Kifungu cha 7(1) (b)** cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilianza uchambuzi kwa kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza Johari (Mb.), siku ya Jumanne tarehe 04 Machi, 2025.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutimiza masharti ya Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati iliwaalika wadau kuwasilisha maoni *(Public Hearing)* kuhusu Muswada huu kwa njia ya kielekroniki au kufika kwenye kikao cha kamati kilichofanyika siku ya Jumatano tarehe 05 Machi, 2025. Kwa upekee Kamati inapenda kuwashukuru wadau wote kwa kutoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada am toa hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo am toa hoja na maoni ya Wadau.

**Aidha,** Siku ya Jumamosi tarehe 08 Machi, 2025 Kamati ilikutana na Serikali ilikufanya majumuisho kuhusu Ibara mbalimbali za Muswada huu kwa kumuhusisha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria na watendaji mbalimbali wa taasisi za Serikali zinazohusika na sheria zinazopendekezwa kurekebishwa na baada ya hapo kwa kuzingatia Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na

kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA
### 2.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Muswada Wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025*) umegawanyika katika sehemu Kuu Kumi (10) na unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Tisa (9) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi wakati Sehemu ya Pili hadi Sehemu ya Kumi zinaweka masharti mbalimbali kwa lengo la kufanya marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria kuu Tisa ambazo ni kama zifuatazo: -

a) Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200
b) Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sura ya 177
c) Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwanda na Majumbani, Sura ya 182
d) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413
e) Sheria ya Hospital ya Taifa Muhimbili, Sura ya 150
f) Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Sura ya 59
g) Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268
h) Sheria ya Sheria ya Bandari, Sura ya 166
i) Sheria ya Sheria ya Utoaji wa Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua mapendekezo hayo yanayopendekezwa kwa kufanya uchambuzi na upembuzi yakinifu kuhusu marekebisho yanayopendekezwa. Baada ya

uchambuzi huo amoja na majumuisho yaliyofanyika baina ya Kamati na Serikali, Kamati hii kama ilivyokuwa kwa wadau mbalimbali, inakubaliana kwa sehemu kubwa na mapendekezo ya Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ilichambua Muswada Ibara kwa Ibara kama zinavyoonekana kwenye Muswada na Wasilisho la Mtoa hoja na kukubaliana na marekebisho hayo isipokuwa kwa Ibara chache ambazo Kamati ilihitaji ufafanuzi na majibu ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi, inayojumuisha **Ibara ya 1** inayohusu jina fupi na **Ibara ya 2** inayoelezea marekebisho yanayopendekezwa kufanyika katika sheria mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua Ibara zote na kubaini Ibara chache zenye hoja za msingi ambazo zilihitaji ufafanuzi kutoka kwa mtoa hoja, Ibara hizo zimechambuliwa hapa chini kama ifuatavyo: -

**2.2 Ibara za Sheria Zenye Mapungufu Zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake.**

**Mheshimiwa Spika**, Wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu Pamoja na Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika sheria Nane kati ya sheria Tisa zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyo wasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hizo ambazo kamati ilizibaini kuwa na mapungufu ni pamoja na:-

i. Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200;
ii. Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwanda na Majumbani, Sura ya 182;
iii. Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413;
iv. Sheria ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, Sura ya 150;

v. Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Sura ya 59;
vi. Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268;
vii. Sheria ya Sheria ya Bandari, Sura ya 166; na
viii. Sheria ya Sheria ya Utoaji wa Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317.

### 2.3 Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika sehemu ya Pili ya Muswada kuanzia **Ibara ya 3** hadi **Ibara ya 4**. Ibara ya 3 inaweka sharti kuwa sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200 wakati Ibara ya 4 ya Muswada inapendekeza kurekebisha **Kifungu cha 26** cha Sheria hii ili kuondoa sharti kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kutoa ridhaa kabla ya kufungua mashtaka ya makosa yaliyoainishwa katika Sheria hii.

Sheria ilivyo sasa, Kifungu cha 26(1) kimempa mamlaka Mkurugenzi wa Mashtaka kwa nafasi yake kutoa ridhaa hiyo na siyo mtu mwingine.

### 2.4 Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika **sehemu ya Nne** ya Muswada kuanzia **Ibara ya 9** hadi **Ibara ya 15**. Ibara ya 14 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 52 kwa kuongeza kifungu cha 52A kinachotoa mamlaka kwa Msajili wa Dawa ya kuweka zuio la muda kwa viuatilifu vya afya ya jamii ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu na mazingira Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ubora na usalama wa viuatilifu vya afya ya jamii vinavyotumika nchini.

### 2.5 Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inahusu ibara za 16 hadi 22 ya Muswada. Ibara ya 17 Inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 5 kwa kufuta majukumu yanayohusiana na uratibu wa shughuli za usalama wa usafiri wa ardhini na uthibitishaji wa ubora wa magari ya huduma za umma na kuipa Mamlaka wajibu wa kuthibitisha ubora wa miundombinu ya reli.

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la Marekebisho ay ani kuondoa baadhi ya shughuli za uratibu kwa kuwa zinasimamiwa na sheria nyingine; kwa mfano kuondoa adhabu zinazotokana na mwendokasi na uthibitishaji wa vyombo vya moto kutumika barabarani unaosimamiwa na Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168. Pia, kuipa nguvu Sheria ya LATRA kusimamia sheria ambazo hazikutajwa katika kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura 413.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 21 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 30 ili kubainisha muda wa kuhudumu kwa wajumbe katika Baraza, ambapo kwa mwenyekiti inapendekezwa kuwa miaka minne na kwa wajumbe kuwa miaka mitatu. Lengo la marekebisho ni kutofautisha muda wa kuhudumu katika baraza ili kutunza na kuhifadhi kumbukumbu za kiutendaji za shughuli za Baraza (Stagger Principle).

### 2.6 Marekebisho ya Sheria ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, Sura ya 150

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inahusu Ibara ya 23 na Ibara ya 30. Ibara ya 23 inaeleza kuwa, Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, Sura ya 150. Aidha, kwa ujumla, Sehemu hii inalenga kuboresha Sheria ya Hospital ya Taifa ya Muhimbili ili Kuboresha ufanisi wa Hospital kuendana na wakati uliopo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Ibara zote zinazofanyia marekebisho Sheria hii, Kamati ilikuwa na hoja katika Ibara ya 29 ambayo inafuta na kuandika upya Kifungu cha 16 cha Sheria ili kuondoa

sharti la lazima kwa Bodi kuwekeza katika uwekezaji unaoruhusiwa katika Sheria ya Uwekezaji wa Wadhamini. Lengo la marekebisho ni kuongeza wigo wa uwekezaji wa hospitali kwa kuzingatia maelekezo yatakayokuwa yanatolewa na Msajili wa Hazina na Mamlaka nyingine zozote zinazohusika.

### 2.7 Marekebisho ya Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Sura ya 59

**Mheshimiwa Spika;** Ibara ya 32 inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 2 cha Sheria ili kuongeza tafsiri ya Msamiati "Medical research" ambalo halikuwepo ili kuongeza uelewa wa maana iliyokusudiwa katika masharti mbalimbali ya Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** dhima kuu ya sheria ni kuanzisha Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Sheria inafafanua maana ya Taasisi na maneno mengine bila ya kutoa maana ya "medical research" katika tafsiri za maneno.

### 2.8 Marekebisho ya Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 43 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 7 (1) (e) kinachohusu kazi za Naibu Mwanasheria Mkuu kwa kuweka neno *"appointment"* kabla ya neno *"discipline"*. Lengo la marekebisho haya ni kumuongezea Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali jukumu la kuteua Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali.

### 2.9 Marekebisho ya Sheria Bandari, Sura ya 166

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 51 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 44 cha Sheria ili kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza Kanuni.

Sheria ilivyo sasa; Kifungu cha 44 (1) kinampa mamlaka Waziri kutengeneza Kanuni na Kifungu cha 44(2) kinaweka Sharti la Kanuni hizo kutangazwa katika Gazete la Serikali ili zipate uhalali wa kutumika.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 53 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 86 kwa kuongeza Kifungu kipya cha 86A ili kuweka adhabu ya jumla kwa makosa ambayo hayajawekewa adhabu mahsusi katika Sheria kuwa isiyopungua Shilingi Milioni Kumi (10) na isiyozidi Shiling Millioni Hamsini (50) au kifungo kisichopungua Miezi Kumi na Mbili (12) na kisichozidi Miaka Miwili (2) au vyote.

Aidha, Sheria ilivyo sasa, katika Kifungu cha 86 cha Sheria hii, haitaji kiwango cha adhabu anachopewa mtu aliyetenda kosa lililoainshwa katika Kifungu hicho, ombwe hii pia inaonekana katika Kifungu cha 66 cha Sheria hii.

### 2.10 Marekebisho ya Sheria ya Utoaji wa Leseni za Usafirishaji, (Sura ya 317)

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 59 zinapendekeza kufuta na kuandika upya Kifungu cha 5 ili kuruhusu Mawakala Waidhiniwa kutoa huduma za utoaji na uhuishaji wa leseni au vibali mtawalia.

**Mheshimiwa Spika**; Sheria ilivyo sasa katika Kifungu cha 5 kinahamisha Mamlaka yote aliyopewa Waziri kisheria ili yasimamiwe na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 67 inapendekeza Kufuta na kuandika upya kifungu cha 46 ili kuipa Mamlaka ya Leseni uwezo wa kukagua Magari ambapo Afisa wa polisi au afisa wa mamlaka, kwa madhumuni ya kuhakikisha utekelezaji wa Sheria hii atakuwa na uwezo wa:-

i. kukagua gari lolote;
ii. kudai kuonyeshwa nyaraka au rekodi yoyote inayotakiwa kubebwa ndani ya gari; na
iii. kumtaka dereva au mtu yeyote aliyepo ndani ya gari kutoa taarifa yoyote anayoihitaji afisa wa polisi.

Lengo ni kuhakikisha kuwa utekelezaji wa majukumu chini ya kifungu hicho yanatekelezwa na polisi na maafisa wa Mamlaka pekee.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata: -

### 3.2 Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200

**Mheshimiwa Spika,** Kwenye Ibara ya 4 ya Muswada Kamati iliishauri Serikali kifungu cha Sheria kibakie kama kilivyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa mashauri yote yanayohitaji ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchi nzima ni lazima yafike kwa Mkurugenzi wa Mashtaka mwenyewe, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho yanayoondoa sharti hilo kwa kuwa yataondoa mlundikano wa mahabusu gerezani.

**Mheshimiwa Spika,** ni maoni ya Kamati kwamba marekebidho haya yamejikita katika misingi ya Haki Jinai ambayo yanaakisi Falsafa ya 4R za **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ambazo ni Maridhiano (*Reconciliation*), Ustahimilivu (*Resiliency*), Mabadiliko (*Reforms*) na Kujenga upya (*Rebulding*).

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa moja ya mkakati Mahususi ya Falsafa hii ni kuimarisha utawala bora, demokrasia na uchumi nchini, kwa **kupitia upya sera na sheria** kwa maendeleo mapana ya Taifa letu. Kamati inakubaliana na marekebisho yanayopendekezwa na mtoa hoja.

Aidha, kutokana na majadiliano yaliyofanyika kati ya Kamati na Serikali, Kamati imeridhia maboresho yabaki kama yalivyo ili

kuondoa tatizo la ucheleweshaji wa haki jinai na mlundikano wa Mahabusu gerezani.

### 3.3 Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182

**Mheshimiwa Spika,** Kwenye Ibara ya 14 ya Muswada Kamati ilipendekeza kufuta neno "may" linaloonekana baada ya neno "Registar" na badala yake kuweka neno "shall". Ili kutoa sharti kwa Msajili kuzuia matumizi ya viuatilifu baada ya kubaini kuwa vinaweza kuhatarisha afya na usalama wa jamii, wanyama au mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea ufafanuzi wa Serikali na kutokana na majibu ya Seriklai Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho kama yalivyotolewa na mtoa hoja.

### 3.4 Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413

**Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 17 Kamati iliomba kupata ufafanuzi wa sababu zilizopelekea Serikali kuondoa majukumu yanayohusiana na uratibu wa shughuli za usalama wa usafiri wa ardhini na uthibitishaji wa ubora wa magari ya huduma za umma na kuipa Mamlaka wajibu wa kuthibitisha ubora wa miundombinu ya reli pekee.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea ufafanuzi wa Serikali na kutokana na majibu ya Serikali Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho kama yalivyotolewa na mtoa hoja.

### Maoni ya Jumla kuhusu Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413

**Mheshimiwa Spika,** ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali itafute suluhu ya mwingiliano uliopo baina ya Tasisi mbalimbali za Serikali zinazosimamia sekta ya usafirishaji kwa njia ya Barabara kama vile Jeshi la Polisi, LATRA, TARURA, TANROADS na TAMISEMI

Mkanganyiko ambao umekuwa ukisababisha kadhia kwa wananchi kwa kutozwa faini na mamlaka tofauti kwa kosa moja. Aidha, muingiliano wa kuitendaji kwa taasisi hizi umekuwa ukififisha jitihada za Mheshimiwa Rais za kuchagiza upatikanaji wa huduma bora kwa Wananchi.

**Pia,** Serikali ifanye rejea ya Sheria ya Sheria zote zinazosimamia LATRA na Jeshi la Polisi ili kuiwezesha LATRA kusimamia udhibiti wa usafiri Ardhini na Jeshi la Polisi kusimamia uratibu wa Usalama barabarani.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuanza matumizi ya mifumo ya kidigitali katika usimamizi wa Sheria za usalama barabarani ili kukabiliana na masuala ya rushwa katika usimamizi na utekelezaji wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, katika Ibara ya 21 inayofanya marekebisho katika Kifungu cha 30, Kamati iliishauri Serikali marekebisho yanayopendekezwa yaakisi mfumo wa kutunza kumbukumbu za kiutendaji za shughuli za Baraza (Stagger Principle) katika Sheria kama.

**Mheshimiwa Spika,** Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.5 Marekebisho ya Sheria ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, Sura ya 150

**Mheshimiwa Spika,** katika Ibara ya 29 ambayo inafuta na kuandika upya Kifungu cha 16 cha Sheria ili kuondoa sharti la lazima kwa Bodi kuwekeza katika uwekezaji unaoruhusiwa katika Sheria ya Uwekezaji wa Wadhamini, Kamati ilipendekeza kufutwa sharti la Bodi ya Hospitali ya Muhimbili kuzingatia maelekezo yatakayokuwa yanatolewa na Msajili wa Hazina na Mamlaka nyingine zozote zinazohusika wakati wa uwekezaji.

**Pia,** Kamati ilikuwa na maoni kuwa, Sheria isimpe mamlaka Msajili wa Hazina ya kutoa ridhaa ya Bodi kuwekeza badala yake Msajili wa Hazina apewe tarifa tu.

**Mheshimiwa Spika,** Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.6 Marekebisho ya Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Sura ya 59

**Mheshimiwa Spika,** Katika Ibara ya 32 Kamati iliishauri Serikali kuboresha tafsiri ya neno "*medical research*" kwa kufuta maneno " *means measuring the health problem, understating its causes, finding solutions or translating the solutions or scientific evidence into policy"* yanayoonekana mwanzoni mwa tafsiri hiyo na badala yake kuweka maneno *"means the systematic study and investigation conducted to understand, prevent, and address health problems, with the aim of improving healthcare outcomes, developing treatments, and advancing medical knowledge or translating scientific evidence into policy,"*.

### Maoni ya Jumla kuhusu Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Sura ya 59

**Mheshimiwa Spika,** ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali iongeze jitihada za ufuatiliaji wa tafiti za dawa za asili zitokanazo na mti shamba katika kukabiliana na magojwa mbalimbali yanayoikabili Jamii. Aidha, Serikali izithibitishe na kuzitangaza kwa jamii dawa za asili ambazo zitakuwa zimekidhi viwango vya ubora kwa matumizi ya matibabu.

**Mheshimiwa Spika,** Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.7 Marekebisho ya Sheria Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268

**Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 43 Kamati ilipendekeza marekebisho ya kiuandishi kwa kuongeza neno "*and*" baada ya neno "*appointment*" ili kuleta maana iliyokusudiwa. Hivyo, kifungu hicho kitasomeka "*appointment and discipline"*

**Mheshimiwa Spika**, Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.8 Marekebisho ya Sheria Bandari, Sura ya 166

**Mheshimiwa Spika,** Kwenye Ibara ya 51 Kamati iliishauri Serikali kufuta aya (f) na (g) ya kifungu cha 44 (2) vinavyopendekezwa na Muswada. Na Ibara ya 53 Kamati iliishauri Serikali kupunguza adhabu ya chini ya faini kwa makosa ya Jumla kutoka Shilingi Million Kumi hadi shilingi Million Tatu. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.9 Marekebisho ya Sheria ya Utoaji wa Leseni za Usafirishaji, (Sura ya 317)

**Mheshimiwa Spika**, Kwenye Ibara ya 59 Kamati iliomba kupata ufafanuzi kuhusu utaratibu wa upatikanaji na utendaji kazi wa mawakala waidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea ufafanuzi wa Serikali na kutokana na majibu ya Serikali Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho kama yalivyotolewa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 67 Kamati ilipendekeza kumuongeza afisa wa Mamlaka katika kipengele (c) cha Muswada ili kumpa uwezo wa kupata taarifa kutoka kwa dereva au mtu aliye ndani ya chombo cha moto cha umma pale inapohitajika ili Kuendana na maboresho ya Sheria yanayopendekezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO
### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na

kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 01. | Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb | –**Makamu Mwenyekiti** |
| 02. | Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb | – Mjumbe |
| 03. | Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb | – Mjumbe |
| 04. | Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb | – Mjumbe |
| 05. | Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb | – Mjumbe |
| 06. | Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb | – Mjumbe |
| 07. | Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb | – Mjumbe |
| 08. | Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb | – Mjumbe |
| 09. | Mhe. Omar Issa Kombo, Mb | – Mjumbe |
| 10. | Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb | – Mjumbe |
| 11. | Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb | – Mjumbe |
| 12. | Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb | – Mjumbe |
| 13. | Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb | – Mjumbe |
| 14. | Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb | – Mjumbe |
| 15. | Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb | – Mjumbe |
| 16. | Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb | – Mjumbe |
| 17. | Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb | – Mjumbe |
| 18. | Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb | – Mjumbe |
| 19. | Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb | – Mjumbe |
| 20. | Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb | – Mjumbe |
| 21. | Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb | – Mjumbe |
| 22. | Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb | – Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ukisaidiwa na Naibu Spika kwa kuliongoza vema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damasi Ndumbaro (Mb.), na Naibu Waziri wake Mhe. Jumanne Abdallah Sagini (Mb.) kwa ushirikiano wao mzuri n awa kipekee walioipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. Kamati pia inampongeza kwa dhati Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Mhe. Hamza Johari (Mb.), akisaidiwa na Mwandishi

Mkuu wa Sheria wa Serikali *(CPD)* Ndg. Onorius Njole kwa kuandaa Muswada huu baada ya kubaini makosa mbalimbali katika Sheria wakati wa utekelezaji wake.

Aidha, Kamati inawashukuru pia kwa ushirikiano walioipatia kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. Kamati inawashukuru pia watendaji wote chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na watendaji wote kutoka taasisi mbalimbali zinazohusika na usimamizi na utekelezaji wa Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa kwa ushirikiano walioipatia Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa niwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka Ildephonce Leonard, kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii; na kwa upekee niishukuru sekretarieti ya Kamati iliyohusika na uratibu wa vikao vya uchambuzi wa Muswada hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025*)** Pamoja na Marekebisho yake, kama ulivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb.
**MWENYEKITI Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala,**
**Katiba na Sheria**
05 Juni, 2025

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Gulamali.

Waheshimiwa wabunge, tunaanza uchangiaji. Tunaanza na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, ajiandae Mheshimiwa Kyombo, ajiandae Mheshimiwa Gulamali na ajiandae Mheshimiwa Kikoyo.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza asubuhi hii ya leo. Naomba kwanza uniruhusu kumpongeza sana Mheshimiwa Hamza Johari, Mbunge na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mara chache sana sisi Wabunge wakati mwingine tunapata fursa ya kutambua mchango mkubwa wa wadau kwenye utungaji wa sheria. Mimi nimekuwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa miaka 10 tukiwa tunafanya kazi hizi na tumefanya kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki kiqfupi ambapo Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria imeshirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali huyu Hamza Johari, tumeona ufanisi mkubwa sana katika utungaji wa sheria. Kwa kweli sisi kama Kamati tunakiri kuwa tumepata mtu mahiri, mtu mwenye weredi wa hali juu na mtu mzalendo sana kwa Taifa lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana na maneno haya kwa sababu hata kwenye hotuba yetu ya Kamati leo mmeona namna ambavyo tumekuwa na mjadala na Serikali kuhusiana na mapendekezo na marekebisho ambayo yaliletwa kwenye Kamati. Unaona kwa sehemu kubwa au kwa 100% tumefikia makubaliano na Serikali katika yale mambo ambayo tuliona kwamba yana maslahi mapana kwa Serikali, Taifa na kwa wananchi, aghalabu kupata watu kama hawa. Tunapowapata ni lazima tuwatie moyo. *(Makofi)*

Ninaomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono katika kupongeza sana sana Mwanasheria Mkuu huyu mzalendo mkubwa sana kwa Taifa letu na ninamshukuru sana kwa sababu amerahisisha sana utendaji wa Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze sana msomaji wa taarifa yetu, Mheshimiwa Seif Gulamali, mtu mzalendo ambaye amekuwa na mchango mkubwa sana kwenye Kamati. Yeye pamoja na Wanakamati wenzetu tumeweza kufanyakazi hii kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na marekebisho ya sheria tisa na mimi ninaomba nijikite kwenye sheria nne kati ya tisa nikiamini kwamba Waheshimiwa Wabunge wengine ambao watapata nafasi ya kuchangia watagusia maeneo mengine ambayo yatabaki na hili ninalifanya kwa sababu ya muda. Ningepata muda wa kutosha tungeweza kuwa na mchango katika kila eneo ambalo limefanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hii Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupanga Sura ya 200 *(The Economic and Organize Crime Control Act Cap. 200)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kuwa miaka ya nyuma uendeshaji wa mashtaka kwa sehemu kubwa, siyo tu yale ya jinai na wala siyo tu yale ya uhujumu uchumi, uendeshaji wa mashataka katika ujumla wake umekuwa ukifanyiwa kwa viwango visivyo na ubora kwa sababu kwa sehemu kubwa uendeshaji wa mashtaka ulikuwa unafanyika kwa watu ambao pengine hawana taaluma hiyo ya kutosha au hawana majukumu hayo kimsingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashtaka yamekuwa yanaendeshwa na polisi ambao ndio wana-*competence* kwenye maeneo ya ulinzi na usalama, lakini kwenye uendeshaji wa mashtaka pengine hawajabobea sana. Katika miaka ya karibuni Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imefanya mapinduzi makubwa sana. Mheshimiwa Rais ambaye kwa nafasi hii tunampongeza sana ametoa fursa ya ajira kwa vijana wetu wenye sifa na uwezo mkubwa ambao wameajiriwa katika maeneo mbalimbali nchini na sasa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inajitosheleza kwa sehemu kwa kuwa na watu wenye weledi wa kuweza kufanya maamuzi na kuendesha mashtaka bila kupata idhini ya moja kwa moja au ya karibu au usaidizi wa karibu wa moja kwa moja wa Mkurugenzi wa Taifa wa Mashtaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo maamuzi haya sasa yanaiondoa ile *section* ya 26 ya hii sheria ambayo ilikuwa inalizimisha kwamba mashauri yanayohusu masuala ya uhujumu uchumi na uhalifu wa kupanga yapate idhini kwanza ya Mkurugenzi wa Taifa wa Mashtaka. Kwa kufanya hivyo, maana yake sasa ni kwamba yale makosa ya uhujumu uchumi yanapotokea kwenye maeneo mbalimbali yanaweza kufunguliwa kwenye maeneo mbalimbali na yakafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, tutapunguza mlundikano mkubwa sana wa mahabusu kwa sababu wengi waliokuwa wakishutumiwa kwa makosa haya walikuwa wanalazimika kushikiliwa kwenye vituo vyetu vya polisi au kwenye mahabusu zetu kwa muda mrefu wakisubiri kibali cha Mkurugenzi wa Taifa wa Mashtaka.

Kwa hiyo, haya maelezo niliona ni maelezo muhimu ili kuwasaidia Watanzania kuona namna gani hii Serikali ya Awamu ya Sita inajitahidi kwa kadri inavyowezekana kupunguza adha inayohusiana na upatikanaji wa haki jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nilidhani nitolee mchango ni sheria mbili; hizi nitazitamka kwa mfululizo kwa kufuatana; kwa maana *The Government Chemistry Laboratory Authority Act Cap. 177* (Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sura ya 177) ambayo kimsingi inaendana sambamba na *Industrial and Consumer Chemicals Management and Control Act Cap.* 182 (Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182).

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia yetu imebadilika sana, wakati hii Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali inatungwa na wakati hii Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Nyumbani inatungwa silaha za kemikali hazikuwa *popular* sana, lakini sasa hali ya dunia imebadilika, aina ya silaha zimeongezeka, ni nyingi. Miongoni mwa silaha ambazo zimeongezeka ni hizi za kikemikali ambazo sheria zetu hizi mbili wakati zinatungwa hazikuliona hilo tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Kemikali ya Mkemia Mkuu wa Serikali inaondoa ile tafsiri ya *chemicals* na inaitaka hii hii sheria sasa itumie tafsiri ya *chemicals* ambayo iko kwenye Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani ili kuweza ku-*accommodate chemical weapons* (silaha za kikemikali). Kwa hiyo, kwa sehemu hii tunaona umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu inaongezwa na nafasi ya mwakilishi kutoka kwenye Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambaye ana utalamu unaohusu silaha za kemikali. Sasa utaona namna ambavyo mapendekezo haya yanakwenda kuliweka Taifa letu katika hali ya usalama zaidi. Kwanza inamuingiza mtu mwenye uwezo wa kutambua, kuchangia na kusaidia kufafanua maeneo yanayohusu silaha za kemikali ambaye ni Askari wa Jeshi la Wananchi mwenye maarifa, weledi na taaluma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili inapanua tafsiri ya kemikali ili kuwezesha kemikali zile ambazo hazikuwepo kwenye orodha ya kemikali hatarishi, zikiwemo hizi silaha za kemikali ziingie kwenye tafsiri zetu za sheria na ziweze kufanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani kwamba hayo ni maeneo muhimu ambayo pia Watanzania wanapaswa kuyaelewa kwa nini sheria hizi zinafanyiwa marekebisho na zina manufaa yapi kwa ulinzi wa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo mengine ambayo yamefanyiwa marekebisho ambapo Kamati imepata nafasi ya kuelezea, lakini kama nafasi inaniruhusu na kama muda utaniruhusu nilitamani niongelee hii Sheria ya Bandari *(The Port Act)* Sura ya 166, nayo imekuja na mapendezo mazuri ambayo nilitamani Bunge lako likubaliane nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za bandari sasa zimezidi kuwa *professional*. Matumizi ya teknolojia yamekuwa ni ya lazima ili bandari yetu iweze kufanya kazi kwa tija na kwa tija kubwa. Sasa ili tufike hapo ni lazima tujali *professionalism*. Kwa hiyo,

mapendekezo yanayoletwa hapa ni kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 12(1) kwa kuongeza majukumu ya bandari kuendesha shughuli za taasisi za mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba bandari sasa iweze kuendesha taasisi ya mafunzo, mafunzo maalum yanayohusu Menejimenti ya Bandari. Mafunzo haya utakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Rais mara kadhaa amelalamika kuhusu mapato na makusanyo yanayotoka bandarini. Moja ya sababu ni kwamba mifumo ya kidigitali haizungumzi, mapato yetu yanavuja, lakini bandari ina fursa nyingi sana. Tunahitaji wabobezi kwenye eneo hili, hatuwezi kuwapeleka kila mahala. Tukiwa na taasisi ya mafunzo maalum kwa ajili ya masuala ya bandari ambayo itaendeshwa na mamlaka za bandari wenyewe tunaweza kuchangia na kusaidia sana Taifa letu katika kubobea kwenye eneo hilo na kupata mapato yatakayoliendeleza Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda ninakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kyombo, wajiandae Mheshimiwa Gulamali na Mheshimiwa Dkt. Kikoyo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa nafasi ya kuchangia katika Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kuipongeza Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mimi kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii na Mjumbe wa Kamati hiyo kwa kweli Kamati imeweza kupitia sheria mbalimbali ambazo Mheshimiwa Rais inampendeza kupitia Serikali yake kuhakikisha kwamba analeta sheria zirekebishwe ili tuweze kwenda na wakati tulionao, lakini tukiwa tunazingatia utashi wake wa kuhakikisha kwamba sheria zote zinakuwa rafiki na zinaweza kutekelezeka ndani ya nchi anayoingoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya pekee nimpongeze sana wakili msomi, Mheshimiwa Hamza Johari kwa utayari wake

na wasaidizi wake. Ni muda mfupi tangu tumeanza kufanya naye kazi kama Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, lakini tunauona weledi wake katika eneo hilo na yeye kwa kweli amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba zile sheria ambazo zinaonekana zina ukakasi katika utekelezaji au zinahitaji maboresho zaidi ili iweze kutumika vizuri; basi amekuwa ikifuata utaratibu wa sheria wa Kiserikali kuhakikisha kwamba zinafika katika Bunge lako Tukufu, na mwisho zinakuja katika Kamati yetu na kuweza kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niendelee kumpongeza na Mwandishi wa Sheria *(CPD),* Onorius Njole pamoja na wasaidizi wake wote. Nichukue nafasi hii ya pekee kwanza kumpongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama ambaye kwa kweli naye amekuwa akituongoza vizuri katika Kamati yetu, kuhakikisha kuwa weledi wake na umahiri unasimama vizuri, hasa kupitia Wajumbe wa Kamati tunapitia sheria hizo zote zinazoletwa ndani ya Kamati yetu tunazipitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatimaye, kwa kushirikiana pia na wadau tunahakikisha kwamba mawazo ambayo ni ya kuboresha yameingizwa ndani ya sheria hizo ili baada ya hapo; baada ya Bunge lako kuridhia na Mheshimiwa Rais akaridhia sheria hiyo basi zije ziwe na tija katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo watangulizi wamesema, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amewasilisha na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu amewasilisha sheria hizi mbalimbali za mwaka 2025. Tunaona Serikali ilikuja na maboresho ndani ya sheria tisa. Tunaona Sheria ya kwanza ni Makosa ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200; Sheria ya pili ni Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Sura ya 177; sheria ya tatu inayorekebishwa ni Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Nyumbani, Sura 182.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna sheria ya nne ambayo inarekebishwa, ni ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini, Sura ya 413; Sheria ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Sura ya 150. Sheria

nyingine ni Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Sura 59. Pia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nayo maboresho yamefanyika. Vilevile kuna Sheria ya Bandari na Sheria ya Leseni ya Usafirishaji, Sura ya 312.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo mahsusi ya sheria hizi zote kama nilivyotangulia kusema yote yamelenga katika kuboresha. Pale ambapo kulikuwa na ulegevu katika kuitekeleza sheria, Serikali ilikuja na maoni ya kuhakikisha kwamba sasa hiyo sheria inaweza ikatekelezeka vizuri ili kuendana na wakati. Sasa tulionao, na hilo ndilo lilikuwa lengo la Serikali. Sisi kama Kamati ni kuhakikisha sasa tunapitia na kwa mara nyingine tunaendelea kuboresha yale malengo mahsusi ya Serikali yaweze kutimia na pia maboresho ya Kamati yapokelewe na Serikali ili kuhakikisha kwamba utekelezaji sasa utakuwa ni mahsusi ndani ya sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo machache tunaangalia, kwa mfano Sheria ya Udhibiti wa Kemikali ambapo Serikali imekuja na maoni mahsusi, lakini tunaona lengo kubwa la eneo hilo ni nini? Ni kudhibiti viuatilifu ambavyo vinaweza kuteteresha afya na usalama wa jamii, wananchi pamoja na wanyama na mazingira tunayotumia. Ukiangalia maudhui unaona kwa kweli ni eneo ambalo linahitaji hii sheria irekebishwe ili sasa tuweze kuhakikisha kuwa tunalinda afya za wananchi, wanyama na pia afya za mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni maeneo ambayo kwa kweli mimi na-*polish* kuonesha Wabunge wa Bunge lako Tukufu, waweze kuridhia kuona hizi sheria zote zimepitiwa vizuri na zinafaa kupitishwa na Bunge lako ili ziweze sasa kwenda katika utaratibu unaofuata, na hatimaye ziwe sheria ziweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaangalia eneo la pili eneo la Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu. Tunaona katika eneo la miti-shamba sisi wote ni mashuhuda. Hapa muda uliopita Mwenyezi Mungu alituokoa katika janga la korona. Tumetumia miti-shamba mingi ambayo na hapa sasa hivi ukiuliza kila mmoja kwamba ni mti-shamba upi ulituponyesha? Kwa hiyo, inatakiwa Serikali sasa, najua imeishaanza kufanyia kazi, ituletee ili tuweze

kuwa na *confidence* na ile miti-shamba iliyotuokoa katika kipindi kigumu ili tuweze kuona kwamba je, hiyo miti-shamba wakati tunatumia katika kipindi cha dharura ni kweli, kile ambacho tulitumia na ikatusaidia. Kisha iweze kuwa *documented* kisayansi na iweze kutumika katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona nchi yetu na wazee wetu tangu nyuma wameendelea kutumia hii miti-shamba. Sasa hii sheria inakuja ili kuhakikisha kwamba sasa inaweza kuweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba hiyo miti-shamba yetu ambayo inatusaidia iweze kuthibitishwa na tuweze kuitumia kwa kuiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo niongelee kidogo ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini; kama Kamati tumepitia na tunaona kazi nzuri zinazofanyika ndani ya Serikali. Hata hivyo, kuna maeneo ambayo yanamuingiliano kidogo. Kwa hiyo, tukaishauri Serikali kwamba ni lazima itoe huu mwingiliano. Zile taasisi zetu zote zinafanya kazi nzuri ya udhibiti katika usafirishaji. Tukiangalia Jeshi la Polisi linafanya kazi nzuri, *LATRA* inafanya kazi nzuri, *TARURA* inafanya kazi nzuri, *TANROADS* inafanya kazi nzuri, lakini pia na TAMISEMI inafanya kazi nzuri, lakini katika kufanya kazi hizo inawezekana kuna maeneo ambayo kunakuwa na mwingiliano ambao huu tusingependa uweze kufifisha juhudi njema za Mheshimiwa Rais ambaye anataka kuleta uchachuzi wa uchumi katika usafirishaji na watu kuongeza na vyombo vya usafirishaji ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Kwa hiyo, maeneo kama hayo tumeona yameendelea kufanyiwa kazi na tunaendelea kusisitiza kama Kamati waendelee kuzingatia maoni ambayo tulitoa kama Kamati ili sheria hizi ziweze kuwa nzuri na ziweze kutumika kwa ufanisi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niombe Bunge lako Tukufu, kwa hizi sheria ambazo zililetwa na Serikali kwa jinsi zilivyopitiwa na Kamati na maoni yote, kwa jinsi tulivyokaribisha wadau mbalimbali kuchangia maoni yao katika kuboresha hizi sheria mbalimbali, ninaomba kwa kweli niwaondoe shaka kwamba tumezingitia ushauri na kuhakikisha kwamba hizi sheria sasa

zikipitishwa na Bunge hili zinaweza kuwa sheria nzuri kwa maslahi ya Taifa na wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maoni hayo machache niombe sasa niunge mkono hoja na kuomba basi Bunge lako Tukufu liweze kupitisha sheria hizi ili ziweze kwenda katika hatua inayofuata ili ziweze kuja kutumika kwa ajili ya maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukushuru na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Gulamali, ajiandae Dkt. Kikoyo.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuweza kupata nafasi tena ya kuweza kuchangia.

Kwanza kipekee nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuruhusu mabadiliko mbalimbali katika nchi yetu katika kuboresha, kutoa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona utayari wa Mwanasheria wetu Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari, mwalimu wangu. Amekuwa ni mwalimu mzuri toka nilipokuwa shule amenifundisha mambo mengi, masuala ya sheria hasa masuala ya *international laws,* lakini leo ninamwona kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali akifanya kazi nzuri na ameleta maboresho mbalimbali kwenye Kamati na pia ndani ya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba sheria zote ambazo zimeletwa na Kamati imeweza kuzichambua kwa kina na tumeweza kuona kwamba lengo la sheria hizi ambazo tumezichambua na kuzipitisha ni kurahisisha kutoa huduma kwa wananchi wetu na kwa wadau mbalimbali ambao wanaozisimamia na wanaozitekeleza, pia zinazoenda kuwahusu wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mimi nipende kutumia fursa hii kumpongeza kwanza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maboresho makubwa kwenye sekta ya sheria ambayo muswada na sheria ambazo zimekuwa zikipitishwa kwa upande wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikuwa inaishia tu kwake akishasaini biashara inakuwa imeisha hapo, hajui kule utekelezaji wa ule mkataba umeenda kutekelezwa kwenye ile taasisi aliyoipitishia mkataba yao, ama Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maboresho haya tunaweza kumpatia nguvu sasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba anapopitisha sheria ya taasisi zozote, ama mikataba yoyote ya kwenye taasisi mbalimbali za Serikali au Serikali kwa ujumla, inampatia nguvu sasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufanya *monitoring* ya kila alichokipitisha kwenye hiyo mikataba mbalimbali katika taasisi za umma pia Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo lake ni nini? Inaisaidia Serikali mikataba inayokuwa imepitishwa kutoka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha kwamba inatekelezwa, inasainiwa kwa wakati, lakini pia inaondoa ule ubadhirifu. Wakati mwingine mikataba imeshasainiwa, baadaye Mwanasheria Mkuu wa Serikali anakuja kuambiwa ule uliopitisha, yameenda kutokea madudu ya wizi na ubadhirifu. Kwa kumpatia mamlaka haya anashuka sasa chini kwenda kufanya *follow up,* kujua hii mikataba imefikia hatua gani, inaendaje, na kama kuna sehemu kuna *mess up* anapata *room* ya kuweza kurekebisha.

Kwa hiyo, ninakupongeza sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuleta haya maboresho ya kukupatia nguvu na bahati nzuri una nyanja zinazoshuka mpaka chini kule katika *level* za wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sheria hizi pia ninakupongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara kwa ujumla kwa kufanya maboresho. Kwa mfano, Ofisi ya *DPP,* hapo mwanzo kila kitu kama makosa ya uhujumu uchumi mpaka yapate kibali kwa *DPP* nchi nzima maana yake unaleta mlolongo mkubwa na kusubirishwa ama kucheleweshwa, kwa hiyo,

usumbufu ulikuwa mkubwa. Leo Ofisi ya *DPP* zipo katika kila wilaya na mkoa. Kwa hiyo, hii inasaidia sasa kuwapatia mamlaka katika *level* za wilaya na mikoa kuhakikisha kwamba kesi za uhujumu uchumi wanapata nafasi ya kuweza kuzipeleka katika Mahakama za Wilaya na Mkoa kwa ajili ya kwenda kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaipongeza sana Serikali kwa kuleta hii miswada ya maboresho na kwenda baadaye kuwa sheria kamili, ili kuboresha na kuongeza ufanisi katika utekelezaji na utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza ambayo nilikuwa ninapenda pia nichangie; kuna Mkataba wa C189 wa Kimataifa. Huu mkataba ni wa kazi za staha za wafanyakazi wa ndani. Huu mkataba umesainiwa na nchi nyingi duniani, lakini bado nchi yetu ya Tanzania hatujasini huu mkataba. Huu mkataba unaenda kulinda haki za wafanyakazi wa ndani wanaofanyakazi ndani ya nchi na wanaokwenda nje ya nchi kwenda kufanya kazi za ndani kwenye nchi mbalimbali. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba na sisi Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Wizara ya Kazi walete huu muswada, pia tusaini huu mkataba na sisi tuingie katika hizo nchi ambazo zimeshasaini. Karibu nchi nyingi duniani zaidi ya nchi 100 zimeshasaini. Sisi bado na hata kuleta hapa bado na kwenye Kamati yetu bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi ikiwezekana kabla ya Bunge hili kwisha, ulete hilo jambo tulitengenezee mazingira, tupitishe ili hawa dada na kaka zetu wanaofanya kazi za ndani, ndani ya nchi na nje ya nchi yetu wawe na sheria ambayo inawalinda ambayo inatambulika kimataifa kama hii ya Mkataba wa C189 ambao umesainiwa duniani kwa wafanyakazi wa ndani ambao wanafanya kazi hizi za kutoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ya kwangu yalikuwa ni hayo ninaomba kuwasilisha. Ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Gulamali ni bora sasa ukasome sheria za michezo hasa mpira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, ajiandae mtoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niungane na wachangiaji waliotangulia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia muda na wasaa wa kujadili haya mambo makuu ya kulijenga Taifa letu, lakini nimshukuru Rais wetu kwa kazi kubwa anayoifanya kuliongoza Taifa letu. Ninawashukuru watendaji wote walioko chini yake na wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na nimpongeze yeye kama yeye kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuboresha sheria zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia kidogo Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi na ninaungana na ninakubaliana na marekebisho waliyoyaleta ya kuondoa takwa la Mkurugenzi Mkuu wa Makosa ya Jinai yanapotokea makosa huko kwenye wilaya zetu, ambayo yalikuwa yanachukua muda mrefu kupata idhini ya Mkurugenzi Mkuu wa Mshataka kabla kesi haijaanza kuendeshwa. Kwa kufanya marekebisho haya ninadhani itasaidia hata kupunguza mrundikano wa kesi kwenye mahakama zetu nchini na watu wakapata haki haraka sana kadri itakavyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, niombe sasa kwa kuwa hii kazi itapelekwa kwenye wilaya zetu, ninajua Serikali ina nia njema kwa wananchi wake, tukaziboreshe sasa hizi ofisi zetu huku kwenye mikoa yetu; na tuhakikishe kwamba pale ambapo ofisi zetu hazijakaa sawa ni muda sasa wa kuhakikisha kwamba tunazipatia vitendea kazi na tunaziimarisha, ili ziweze kufanya hii kazi ambayo ni ya kutoa haki. Kwa sababu wanasheria tunasema haki iliyocheleweshwa ni sawasawa na haki iliyokataliwa. Sasa ili haki iharakishwe tukaziboreshe na kuzipatia vitendea kazi vya kutosha, ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza pia Serikali kwa kuja na haya maboresho ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali Viwandani hasa kwa kumpatia Msajili kuongeza kifungu cha 52A ambacho sasa kinampatia mamlaka Msajili wa Hazina, aidha, kukataa kuruhusu kemikali kuingia nchini, endapo atajiridhisha kwamba hizi kemikali hazina manufaa kwa matumizi ya binadamu na mimea hasa kwenye nchi yetu. Tusije tukawa kila kitu kinachoingia tunaingiza tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa na Ofisi ya Msajili tuwapatie mafunzo kwenye haya masuala ya kemikali, waweze kulisaidia Taifa letu lisijekuwa kila kitu kinaingia na kinaharibu mazingira yetu na afya za watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Sheria ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini ninashukuru kwa marekebisho yaliyofanywa. Tunapoongelea Sheria ya Udhibiti ya Usafiri Ardhini ni sheria mtambuka na ni sheria muhimu sana kwa mustakabli wa uchumi na maisha ya watu wetu. Hakuna sekta ambayo ukiamka lazima uitumie ni sekta hii na inatumiwa na watu wengi. Kwa hiyo, maboresho ambayo yamefanyika na niombe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, sheria hii tuifanyie marejeo mara kwa mara kwa sababu inagusa maisha ya watu wetu hasa wenye kipato cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwamba tumeliangalia Baraza la *LATRA,* tumefanya marekebisho pale, Wajumbe wa Baraza wameainishwa, Mwenyekiti atateuliwa na Waziri. Mwanzoni ilikuwa ni shida na ninaomba ni-*declare interest,* nimefanya kazi kwenye hilo Baraza ilikuwa ni shida kweli kweli. Wanateuliwa Wajumbe wa Baraza mnaanza kutafuta Mwenyekiti. Kuna kipindi tulishindwa hata kupata Mwenyekiti, lakini ninashukuru kwa marekebisho yaliyofanywa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba sasa Mwenyekiti atateuliwa na Waziri, hicho kipingamizi kimeondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza limepewa muda tofauti wa Wajumbe kumaliza muda wao *(staggering board)*, lakini wakati tunajadili hii sheria ninadhani Mheshimiwa *AG* utakumbuka mimi nilikuja na pendekezo binafsi kwamba kwenye hii sheria

tumeainisha baraza, tumeongelea mambo ya Sekretarieti lakini tukasahau *financing model* ya hili baraza. Niombe Mheshimiwa *AG* utakapokuja kutoa maelezo ya mwisho utuambie ni lini ambapo kama Serikali mnadhani hili baraza tulipatie nguvu ya kufanya kazi yake, tulipatie na vyanzo vinavyoaminika vya mapato, ili liweze kufanya kazi kwa ufanisi na kwa lengo ambalo lilikuwa limekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sheria hiyo hiyo ninakushukuru kwamba tumeweza sasa kutoa kwenye mabadiliko yaliyoletwa hasa kipengele cha tano cha Sheria ya *LATRA* kwamba sasa bodi ikatafuta mawakala huko kwenye wilaya zetu hasa vijana wetu wanapokuja kuomba leseni, ni jambo jema, lakini tuangalie isije ikawa matatizo tuliyokuwa nayo kwenye Jeshi la Polisi hasa Kikosi cha Usalama Barabarani tukaanza kutengeneza vishoka kule. Lengo ni jema, katika utekelezaji huo tuhakikishe kwamba tusije tukaongeza matatizo ya vishoka hasa kwa wale mawakala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu wakati inatoa maoni imetoa maoni ambayo ninaomba nisome; "Maoni ya Kamati; Serikali itafute suluhu ya mwingiliano uliopo baina ya taasisi mbalimbali za Serikali zinazosimamia sekta ya usafirishaji."

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya sekta ambazo zina taasisi nyingi, majukumu yao yanaingiliana na ndiyo maana tuna matatizo kwenye sekta ya usafirishaji. Nimwombe Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tuliangalie hili, majukumu ya usafirishaji yamebebwa na taasisi nyingi na Wizara nyingi na zote zinaingiliana na zinafanya kazi pamoja, hakuna kiranja. *LATRA* inasimamia usafiri wa ardhini, lakini tuna Kikosi cha Usalama Barabarani, Sheria ya *Road Traffic,* tuna mamlaka za halmashauri zetu kule, lakini tuna *TRA,* leseni zetu za kuendesha magari zinatolewa na *TRA,* lakini stendi nyingi zinamilikiwa na halmashauri zetu na Tuna Kikosi cha Usalama Barabarani, ukiangalia pale kuna mkanganyiko ambao hauna afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri masuala yote yanayohusiana na usafiri wa ardhini yawe chini ya mamlaka moja kama ilivyo usafiri wa anga na wa majini. Tuwe na taasisi moja

ipewe majukumu yote, ili tuweze kuiwajibisha pale ambapo tunapata matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyoongea, Jeshi la Polisi lipo barabarani linafanya kazi ya udhibiti wa usafiri ardhini. Kazi yao ibaki kwenye *enforcement* peke yake. Masuala ya udhibiti tuyaachie Mamlaka ya Udhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nipongeze kwa marekebisho yaliyoletwa kwenye Mamlaka yetu ya Bandari. Nchi yetu ni lango la nchi kama tano hivi ambazo zinategemea bandari yetu. Mamlaka yetu ya Bandari imekuwa ikiendesha shughuli zake za kibandari kwa ufanisi mkubwa sana. Ninashukuru kwenye haya mabadiliko kwamba ikasimamie na kutunga kanuni za taasisi ambazo zipo chini yake hasa shule yake au chuo chake cha bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari yetu tunavyoongea leo ni *generation* ya tano (uzao wa tano), lakini duniani huko wameshakwenda mpaka *generation* ya sita. Sisi bado tupo *generation* ya tatu. Mheshimiwa Mhagama amesema, tunahitaji kufanya utafiti ili tutoke hapa tulipo, na tutokaje hapa tulipo ni kuhakikisha vijana wetu wamesoma lakini tumewekeza kwenye bandari yetu, ili tutoke kwenye *generation* ya tatu, twende kwenye *generation* ya nne, tano na sita. Dunia inakimbia na muda unakwenda, lakini bandari kwa uchumi wa Tanzania tunaita *cash cow*. Soko lipo, tunachohitaji ni kujidhatiti, tutunge sheria zetu ziendane na wakati tulionao ili bandari zetu tuziimarishe. Vilevile sheria hizi zinazohusiana na masuala ya usafiri na usafirishaji tuziboreshe mara kwa mara ziendane na muda na teknolojia iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana na ninaunga hoja mkono. Ninawapongeza Watendaji wa Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mtoa hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa

Wabunge ambao wamechangia katika hoja hii iliyopo mbele yetu. Kwa heshima na taadhima nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mheshimiwa Seif Gulamali na Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo kwa michango yao mizuri, lakini pia ninawashukuru kwa pongezi zao kwangu. Niseme tu kwamba pongezi zenu zimezidi kunitia moyo wa kuchapa kazi. Kwa hiyo, nitaongeza bidii ya kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michango yao ni muhimu sana kwa ajili ya kupanua uelewa wa maudhui ya marekebisho ambayo tumekuwa tumeyapendekeza hapa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utungaji wa sheria hii muhimu sana, lengo letu lilikuwa ni kuhakikisha kuwa malengo na madhumuni ya Bunge ya kutunga au kurekebisha sheria yanaeleweka kwa ufasaha ili kurahisisha utekelezaji wake. Hivyo, michango ya Waheshimiwa Wabunge ni ya muhimu sana kwa kuwa inasaidia kuweka bayana katika Kumbukumbu za Bunge lako Tukufu malengo ya Bunge *(intentions of the Parliament)* katika sheria au marekebisho husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza wakati wa kuwasilisha muswada, lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuboresha sheria zetu ili ziendane na mahitaji ya sasa ya kijamii na kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanazuoni mmoja ambaye pia alikuwa ni Mwanasheria na Mbunge katika Bunge la Wawakilishi la Marekani *(US House of Representative)*, miaka ya 1915 – 1919 aliwahi kusema kama ifuatavyo na nitanukuu na nitajaribu kutafsiri, alisema kwamba; *"Laws and institutions must go hand in hand with progress of human mind. As that becomes more developed, more enlightened, as new discoveries are made, new truth discovered, and manners and opinions change with change of circumstances. Institutions must advance also to keep pace with the times. When we might as well require a man to wear still the coat which fitted him when a boy as civilized society to remain ever under the regimen of their barbarous ancestors."*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajaribu kutafsiri alichokuwa anasema Mwanasheria James Jefferson kwamba; "mfumo wa kisheria na kitaasisi ni lazima uende sambamba na maendeleo na ukuaji wa fikra za mwanadamu. Kadri binadamu anavyoendelea kuelimika, uvumbuzi mpya unavyoendelea kufanyika, na mitazamo pamoja na mienendo ya kijamii kubadilika kutokana na mazingira mapya ndivyo ambavyo mifumo ya kisheria na kitaasisi inapaswa pia kubadilika ili kuendana na mahitaji ya wakati. Kuzuia mabadiliko katika mfumo wa sheria na taasisi ni sawasawa na kumlazimisha mtu mzima kuendelea kuvaa koti alilovaa alipokuwa mtoto na kuiweka jamii ya kisasa chini ya utawala wa desturi za mababu zao waliokuwa katika hatua za awali za ustaarabu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni jambo la kimkakati kuhakikisha kwamba sheria zetu tunaendelea kuhakikisha kwamba zinanyumbulika na maendeleo ya Taifa hili. Kwa hiyo, ni kazi ambayo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaipa kipaumbele namba moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango hii mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge tangu wakati wa Kamati tutaizingatia. Kwa sababu ni kazi ambayo tumedhamiria kwa dhati kabisa kuhakikisha kwamba sheria zetu zinaendana na kadri maendeleo yanavyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hivi karibuni tumezindua Dira ya Maendeleo ya mwaka 2050. Tuna kazi kubwa ya kufanya tunaelewa, tunajua kwamba tuna sheria nyingi sana tutahakikisha kwamba tunazifanyia mabadiliko ili tuweze kufika huko tunakotaka kufika kadri Dira yetu ya 2050 ilivyotuelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Seif Gulamali amezungumzia Mkataba wa Kimataifa wa Shirika la Kazi Duniani yaani maarufu kama *ILO Convention* wa 189 *(ILO Convention 189)*, maarafu sana kama *C189*. Mkataba huu wa Kimataifa una lengo la kuweka viwango na masharti pamoja na haki za wafanyakazi wa majumbani yaani *domestic workers*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, umeweka masharti yote ikiwemo kuhakikisha kwamba wafanyakazi hawa wanakuwa na mikataba ya kazi, wanalipwa stahiki zao vizuri, wanalipwa mishahara vizuri, lakini wanakuwa *treated* kama wafanyakazi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama alivyosema, nikiri mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hatujaridhia mkataba huu na hilo ombi alilolisema ni la msingi na ni muhimu kwa sababu wafanyakazi hawa wapo katika Sekta yetu ya Kazi. Kwa hiyo, ni vizuri mikataba hii ya Kimataifa na yenyewe tukaitambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kushirikiana na waziri mwenye dhamana na mambo ya kazi, basi tutashauriana kuhakikisha kwamba tunaridhia mkataba huu, unaletwa kwenye Bunge lako Tukufu ili tuweze kuridhia ili hawa wafanyakazi wa majumbani basi hizo haki zao, stahiki zao, mikataba yao inakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimshukuru sana Mheshimiwa Seif Gulamali kwa michango yake hiyo mizuri. *ILO Convention 189* ni mkataba muhimu na tutafanya litakalowezekana ili kuhakikisha kwamba tunauridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Kikoyo kwa michango yake mizuri, lakini ametusisitiza tuhakikishe kwamba Sheria ya *LATRA* yaani Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini inafanyiwa marekebisho mara kwa mara. Hilo tumelichukua na tutahakikisha kwamba sheria hii inakuwa inafanyiwa marekebisho kadri pale mahitaji ya kufanya hivyo yanapohitajika kwa kushirikiana na Wizara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile amezungumzia kuhusu Baraza la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Ardhini kwa maana ya *LATRA CCC*, akisisitiza kwamba baraza hili tuangalie yaani kama Serikali tuangalie namna gani tutaliwezesha katika masuala ya kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri katika Bunge lako, siyo *LATRA CCC* tu peke yake ambayo ina changamoto hizo, bali na mabaraza mengine ya kisekta kama haya kama vile *EWURA CCC*, *TCRA CCC*, *TCAA CCC,* yote yana changamoto zinazofanana. Kwa hiyo, kwa kushirikiana na Waziri wa Kisekta wa mabaraza yote haya pamoja na hili tutaangalia namna gani tunaweza kutatua suala la changamoto za kifedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tutaendelea kuhakikisha kwamba hizo mamlaka za udhibiti katika hizo sekta zinaendelea kuyatunza na kuyapa fedha ili yaweze kujiendesha kipindi hiki ambacho bado hatujaweza kuwa na mfumo thabiti wa kifedha wa uendeshaji wa mabaraza haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ametupongeza kwenye suala hili la sasa kuruhusu mawakala nao kushughulika katika masuala ya shughuli za usafiri wa ardhini, lakini ametoa angalizo pasijekutokea tena vishoka. Kwa hiyo, hilo nafikiri tulipokee kama Serikali na kwa kushirikiana na Wizara ya Uchukuzi tutalifikisha ili wahakikishe kwamba jambo hilo halileti changamoto hizo ambazo umezitolea wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala la mwingiliano katika Wizara ya Uchukuzi, ni kweli hasa katika taasisi hii ya *LATRA*. Kwa hiyo, na lenyewe tulichukue ili waweze kulifanyia kazi kwa maana ya kwamba mamlaka ya utoaji wa leseni katika usafiri wa ardhini uwe chini ya taasisi moja. Hapa amejikita zaidi kwenye *Personnel Licensing Function* ya *LATRA* kwamba iwe *more improved* na isiwe inatolewa katika taasisi tofauti tofauti, akitolea mfano wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali nalifahamu vizuri na sheria hizi za udhibiti ni mbobezi, kwa hiyo, tutashirikiana na Wizara ya Kisekta kuhakikisha kwamba jambo hili linarekebishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa niwashukuru wote ambao wamechangia na tumeona kwamba kwa kazi nzuri tuliyoifanya wakati wa Kamati na kwa kuwa tulikuwa tunashirikisha wadau wengi na kwa kuwa tulikuwa wasikivu kila pale ambapo

ushauri tuliokuwa tunapewa na Kamati tunauzungatia, na marekebisho haya yanayopendekezwa ni zao la kazi nzuri tuliyoifanya kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Kamati, lakini na Wizara za Kisekta, imepelekea kwamba tusiwe na hoja nyingi sana siku hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwashukuru sana Kamati, lakini niwashukuru Mawaziri wote na watendaji wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwezesha kazi hii kuwa nyepesi na tumeweza kuifanya kwa weledi mkubwa na leo hii tunavyohitimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango mizuri. Tumepokea maoni mazuri ambayo yanalenga kuboresha si Muswada tu, bali hata masharti mengine ya sheria mama, lakini pia vilevile yatasababisha na kuangalia sheria zingine ambazo zinashabihiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni ushahidi kwamba suala la marekebisho ya sheria kwa lengo la kuboresha utekelezaji madhubuti wa sheria zilizopo linamhusu kila mmoja wetu katika Bunge hili, na ni jambo litakalokuwa endelevu katika Bunge hili katika kuhakikisha kwamba sheria zetu zinanyumbulika na kasi ya maendeleo ya Taifa hili na ndiyo maana kila mwaka Serikali tunakuja na muswada wa aina hii ili kuboresha masharti ya sheria zetu na kuzifanya ziendane na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, kwa mara nyingine tena niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote. Nikushukuru na wewe binafsi Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Spika na watumishi wote wa Bunge, Katibu wa Bunge, kwa msaada mkubwa waliotupa wakati tunaandaa muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa heshima na taadhima ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeunga mkono.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17

Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 32

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 43
Kifungu cha 44

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48
Kifungu cha 49
Kifungu cha 50

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 51

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 52

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 53

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 54
Kifungu cha 55
Kifungu cha 56
Kifungu cha 57
Kifungu cha 58
Kifungu cha 59
Kifungu cha 60
Kifungu cha 61
Kifungu cha 62

Kifungu cha 63
Kifungu cha 64
Kifungu cha 65
Kifungu cha 66

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 67

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 68

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya mpangilio wa vifungu kutoka 45 hadi 68 kuwa kifungu cha 46 hadi 69.
Kifungu cha 69

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023 napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya

Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2025)* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2025)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO JAMII, JINSIA, WANAWAKE, NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya Mwaka 2025 pamoja na marekebisho yake. Walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa Ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali Zipatazo Tisa kwa Lengo la Kuondoa Mapungufu ambayo Yamejitokeza Wakati wa Utekelezaji wa Baadhi ya Masharti katika Sheria Hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in Order to Keep the Laws Updated with Some Challenges Observed in Its Implementation)***

*(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muswada kwa mujibu wa kanuni zetu na sheria zetu ukishwasomwa mara tatu kwa maana hiyo muswada sasa umepita. Hongera sana *AG,* kazi hii

unayoifanya siyo ndogo, ni kazi kubwa sana na Tanzania siyo kisiwa, lazima tuendane na dunia kubadilisha sheria zetu kwa maslahi ya nchi yetu na taratibu za Taifa letu. *(Makofi)*

Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kila ambapo naona kuna umuhimu wa kulipeleka mbele Taifa letu lazima tuendane na sheria zetu kwa maslahi ya Taifa letu. Hongereni Wabunge na Kamati kwa michango mizuri, wataalam mnaomsaidia *AG* na ninyi hongereni sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno haya niwashukuru tena. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 6.36 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 6 Juni 2025 Saa Tatu Asubuhi)*